


UKURASA 11

**RAIS** Dk. Mwinyi: Siachi kubomoa, kujenga upya Mji Mkongwe

UKURASA 3



**MABILIONI** kujenga magati sita bandari za Dar, Bagamoyo

UKURASA 5

**WAZIRI** Elimu apiga marufuku michango ya lazima shuleni

UKURASA 5


# Nipashe

Jumatano Januari 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581551

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newsr


UKURASA WA 7

## HOSPITALI YA TUMBI YATAKIWA KUIMARISHA DAWATI LA MAONI

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Jingu ameagiza Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani (Tumbi) kuimarisha njia za kupata mrejesho kutoka kwa wanaowahudumia. Ametaka kuwapo mfumo rasmi utakaojulikana kwa...

UKURASA WA 24


## BENCHIKHA SASA AMNYIMA USINGIZI CHASAMBI SIMBA

WINGA mpya wa Simba, Ladack Chasambi, amesema anatambua kuwa amejiunga na timu yenye wachezaji wakubwa na anatarajia kupata ushindani mkubwa wa kuwania namba, lakini atahakikisha anajituma mazoezini kwa ajili ya kumshawishi Kocha...



# Kilichojificha kuandika matusi kwenye mtihani

UKURASA 4



Wanafunzi wakifanya mitihani. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Samia aonya uchepushaji karafuu



UKURASA 2

## SHERIA UCHAGUZI

## Kamati Bunge: Hoja za kujadili ni zisizovunja Katiba tu

UKURASA 2

**MICHEZO** GAMONDI APEWA PANGA YANGA UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaabani, pamoja na viongozi mbalimbali wakati akikata utepe kuashiria ufunguzi wa jengo la Kitega Uchumi la Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) lililopo Chakechake Pemba jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia aonya uchepushaji karafuu

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaonya wakulima wa karafuu kuhusu uchepushaji na uuzaji magendo zao hilo kwa kuwa wanaofanya hivyo wanafifisha maendeleo yao.

Akifungua jengo la Kitega Uchumi la Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC) Chake Chake, kisiwani Pemba jana, Rais Samia alisema wanapopima maendeleo ya uchumi, sekta ya kilimo wanaiona iko juu kwa sababu ya karafuu.

Aliwataka wakulima kuendelea kulima karafuu kwa wingi na kwa tija zaidi ili kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuinua uchumi wa buluu.

Alisema serikali itaendelea kutafuta fursa za kuongeza tija na uzalishaji bila kuathiri viwango na thamani ya karafuu katika soko la kimataifa.

"Suala la magendo ndugu zangu tuliache na tuiachie serikali ifanye kazi yake. Sasa Karafuu inanunuliwa kisayansi, ile enzi ya kuipima kwa mkono ukamwambia mkulima, 'Karafuu yako ina unyevu mkubwa gredi yake ya pili' sasa dhuluma ile haipo, sasa kila kitu ni mashine, kupima na kuisafisha.

"Sasa Karafuu inayotoka Zanzibar kwenda nje ni safi na yenye viwango vya hali ya juu kiasi ambacho, tunakwenda kulitawala soko la Karafuu ulimwenguni, na hii ni hatua kubwa," alisema.

Rais Samia aliwasisitiza wakulima kuendelea kulima karafuu kwa wingi na kwa tija zaidi ili kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuinua uchumi wa buluu. Alisema kimataifa Zanzibar imekuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa zao hilo.

Alisema serikali itaendelea kutafuta fursa za kuongeza tija na uzalishaji bila kuathiri viwango na thamani ya karafuu katika soko la kimataifa.

Rais Samia aliiagiza ZSTC kutatua kero za wakulima pamoja na kuwa na kanzidata ili kutunza kumbukumbu za zao hilo na wakulima zitakazowezesha kuratibu mipango endelevu.

Aliitaka ZSTC kutumia ipasavyo jengo lililozinduliwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwamo kukusanya mapato yatakayosaidia kujiendesha yenyewe na kupunguza gharama kwa serikali.

"Hapa jengo hili ni kitega uchumi kwa hiyo matumaini yangu ni kwamba, Shirika la ZSTC watalitumia jengo hili vyema kutafuta fedha ambazo haitalazimisha sasa hazina ya serikali kutoa fedha kuwapa shirika.

"Zao la karafuu limeendelea kuwa na umuhimu kwa uchumi na maendeleo yetu Zanzibar, ni moja kati ya zao kongwe sana katika visiwa vyetu, na tunaweza kusema ni almasi yetu Zanzibar. Hatuna budi kuitunza, kuienzi na kuiendeleza," alisisitiza.

Pia alisema toka wakati wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, zao hilo limeendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa eneo hilo na kwamba, hadi sasa linashikilia namba moja katika mauzo ya Zanzibar nje ya nchi.

Alisema mwaka 2022 mauzo ya karafuu nje ya nchi yalichangia Sh. bilioni 118, sawa na asilimia 65.6 ya mauzo yote ya Zanzibar yanayouzwa nje na kwamba kupitia zao hilo, Unguja na Pemba zimejipatia jina maarufu la visiwa vya marashi ya karafuu.

Alisema maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi cha Chama cha Mapinduzi ya 2020/25, ni kuongeza uzalishaji wa karafuu hadi kufikia tani 10,000, huku hatua kadhaa zikichukuliwa ili kufikia malengo hayo.

"Serikali imeendelea kuimarisha bei ya karafuu ili kuendana na soko la kimataifa. Kwa msimu ulioanzia mwezi Agosti, 2023, bei kwa kilo ya karafuu ya daraja la kwanza, ilipanda kutoka Sh. 14,000 hadi 15,000 na kupitia ongezeko hilo, inakisiwa Sh. bilioni 76.4 zinakwenda kwa wakulima na wameshafaidi na fedha hizo," alisema Rais Samia.

Alisema wakati wanalenga kuongeza kiwango cha uzalishaji shabaha yao iwe kuongeza tija ya uzalishaji katika kila hekari.

Rais Samia alisema kwa sasa wastani wa uzalishaji ni tani 1.4 kwa hekari, wakati nchi nyingine zinazalisha tani 1.8.

Aliahidi kuwa serikali itaendelea kutafuta fursa za kuwaongezea wakulima ujuzi na utaalamu ili waendelee kuongeza tija na ubora kwenye kilimo cha karafuu nchini.

"Angalizo langu katika hili ni kwamba, tunapotafuta njia za kisayansi za kuongeza tija na uzalishaji tusishushe hadhi na ubora wa karafuu yetu.

"Tunaweza kupata wataalamu wa sayansi wakatuongezea uzalishaji, lakini hadhi ya karafuu yetu ikashuka, hivyo tusishushe ubora wetu kwa sababu ya kuongeza tija," alisisitiza Rais Samia.

Pia alitoa wito kwa ZSTC kuendelea kuwa karibu na wakulima kwa kuwapa nyenzo za kisasa, kutatua kero zao, kuwapa ushauri wa kitaalamu na kuwa na kanzi data inayoonyesha ukubwa wa shamba na makadirio ya mavuno.

Alisisitiza kuwa makadirio ya zao hilo yasifanywe kwa kichwa badala yake, ufanywe kisayansi ili wawe na uhakika wa watakachokwenda kuvuna na mipango ya maendeleo katika bajeti zao.

Rais Samia alishauri shirika kuingia mkataba na wakulima katika mashamba ya serikali.

Katika hatua nyingine, serikali ya Zanzibar imetia saini mkataba wa ujenzi wa Bandari ya Maruhubi na kampuni Devco kutoka Uholanzi, huku Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, akishuhudia na kusema bandari hiyo mpya ni fursa kubwa kibiashara, kiuchumi na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Hafla hiyo ilifanyika jana katika viwanja vya Ikulu. kwa upande wa Zanzibar saini hiyo iliwekwa na Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Khamis na kwa kampuni ya Devco ikitiwa na Mtendaji Mkuu wake, Matthew Vander Borgh.

# 'Maoni miswada ya sheria ni yasiyovunja Katiba ya nchi'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria, Joseph Mhagama, amesema maoni ya miswada ya sheria za uchaguzi yatakayofanyiwa kazi ni yale ambayo hayavunji Katiba ya nchi.

Mhagama, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini mashirika pamoja na taasisi mbalimbali wakati akipokea maoni kutoka kwa makundi hayo kuhusu miswada minne ya uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Alisema wakati huu wadau wanapoendelea kutoa maoni yao kuhusu miswada ya sheria ya uchaguzi pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Kamati yake itafanyia kazi ambayo yatakuwa hayavunji Katiba ya nchi.

"Kama kamati tutafanyia kazi maoni yale tu ambayo hayavunji katiba yetu hivyo nitoe wito kwa wadau wote ambao watapata fursa ya kutoa maoni yao kutoa yale ambayo hayavunji Katiba ya nchi," alisema.

Mwanasheria wa Jumuiya ya Kikristo (CCT), Gloria Mafole, akitoa wasilisho na maoni ya jumuiya hiyo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, alisema wanapendekeza kuondolewa kwa kifungu ambacho kinataka mtu atakayepoteza au kuharibu kitambulisho achangie kiasi cha fedha ili kutengenezewa kipya.

"Tunapendekeza kifungu hichi kuondolewa kwenye sheria ya uchaguzi wa urais, wabunge pamoja na madiwani kwani hali hii itasababisha wananchi kupunguza ushiriki katika uchaguzi, lakini kifungu kingine ni kuondolewa kwa dhamana ya watu wanaogombea nafasi ya urais kwani dhamana ya chama peke yake inatosha," alisema.

Pia alisema wanapendekeza Sheria ya Uchaguzi kuweka ukomo wa idadi ya wabunge kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa na jukumu la kusimamia majimbo yaliyopo bila kuathiri idadi hiyo.

Mwenyekiti mstaafu wa Umoja wa Madhehebu ya Kipentekoste nchini (CPCT), Askofu Peter Konki, aliwashauri wadau mbalimbali waliopata fursa ya kutoa maoni yao wajikite kwenye mambo ambayo yataendelea kujenga umoja wa kitaifa.

"Fursa hii tuitumie vizuri ili kutoa maoni yetu kwa lengo la kuwa na umoja wa kitaifa badala ya kutoa vitu ambavyo vitatuondolea umoja wetu na kutugawa," alisema Askofu Konki.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo (CCT), Askofu Fredrick Shoo, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu mchakato wa kutungwa sheria za uchaguzi ambazo zitasaidia kuongeza demokrasia nchini.

"Sisi CCT tumepata mwaliko wa Kamati kuja kutoa maoni yetu tumetoa ambayo yatasaidia kuboresha miswada hii ya sheria na tunaomba wadau wengine kuendelea kutoa maoni yao ambayo yataendelea kulinda umoja wetu wa kitaifa badala ya kutugawa," alisema Askofu Shoo.

**HABARI KITAIFA**

# Mkulima kizimbani mashtaka kuiba milioni 159.5/- za benki

**Na Grace Gurisha**

MKULIMA Respicius Magesa (52) amepandishwa kizimbani kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, akishtakiwa kutoa Sh. milioni 159.5 kutoka akaunti binafsi ya Benki ya CRDB ya Dola za Marekani na kuziingiza katika akaunti ya Shule ya Sekondari Macmillan kwa njia ya udanganyifu.

Mbali na Magesa, washtakiwa wengine ni Dereva wa CRDB, Michael Owiti (43); wafanyakazi wa benki, Sia Meta (36) na Ray Nittu (38); wafanyabiashara Aisha Bagasha (38), Deogratius Rulangalanga (43), Andrew Kamugisha (45) na Ezekiel Salakana (38), wote wakazi wa Dar es Salaam.

Washtakiwa hao waliomba mahakama iwape nafasi ya kufanya mawasiliano ili wawape taarifa ndugu zao kwamba wamekamatwa na wamepelekwa gerezani kwa sababu hakuna mwenye taarifa ya kupandishwa kizimbani.

Akisoma hati ya mashtaka jana, Wakili wa Serikali Aron Titus, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Aaron Lyamuya, alidai washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka sita ya uhujumu uchumi, kuongoza genge la uhalifu, kuingilia mfumo wa kompyuta, kughushi, kuwasilisha nyaraka ya uongo, kujitambulisha na kutakatisha fedha.

Wakili Titus alidai kuwa katika shtaka la kwanza la kuongoza genge la uhalifu linalowakabili washtakiwa wote, inadaiwa kati ya Julai 20, 2023 na Oktoba 29, 2023, washtakiwa, wakiwa maeneo tofauti ndani ya Dar es Salaam, kwa nia ovu waliongoza mtandao wa kihalifu kwa kufanya vitendo vya udanganyifu na kujipatia Sh. milioni 159.5.

Alidai kuwa katika shtaka la pili linalomkabili mshtakiwa wa tatu (Nittu), anadaiwa kughushi kupitia mtandao wa kompyuta akiwa ni Ofisa Mauzo wa Benki ya CRDB Tawi la Mwenge Julai 20, 2023, aliingilia mfumo wa kompyuta kwa kuonesha kuwa Kepha Mwiti amebadilisha taarifa zake za benki kwenye akaunti yake binafsi.

Inadaiwa kuwa lengo lake ilikuwa taarifa hizo alizobadilisha zifanyiwe kazi na kwamba taarifa hizo ndiyo sahihi wakati akijua taarifa hizo ni za uongo.

Ilidaiwa kuwa Septemba 9, 2023, Magesa akiwa benki ya CRDB Tawi la Kibada, Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, kwa nia ovu aliandaa taarifa za uongo (Deposit Withdraw Slip-Cash Only) ya tarehe hiyo akiwa na lengo la kuonesha Mwiti alitaka kutoa Dola za Marekani 19,200 kwenye akaunti yake binafsi katika Tawi la Mikocheni.

Alidai kuwa fedha hizo ziingizwe kwenye akaunti namba 0150460392500 yenye jina la Shule ya Sekondari Macmillan iliyoko Tawi la Quality Center huku akitambua kuwa si kweli.

Pia anadaiwa kuwasilisha nyaraka hizo CRDB akionesha Mwiti anataka kutoa fedha hizo wakati akijua si kweli.

Katika shtaka la tano, Magesa anatuhumiwa Septemba 9, 2023, akiwa Tawi la CRDB Kibada, Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, alijiwasilisha mwenyewe kuwa ni mmiliki wa akaunti ya Mwiti kwa ofisa wa benki Stephen Mponeja wakati akijua si kweli.

Alidai kuwa katika shtaka la sita la utakatishaji fedha, linalowakabili washtakiwa wote, wanadaiwa kuwa kati ya Julai 25 na Septemba 29, 2023, wakiwa ndani ya Dar es Salaam, walijipatia mali ambayo ni mazalia ya uhalifu wa kughushi nyaraka na kujipatia Sh. milioni 159.5.

Wakili Titus alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

Baada ya washtakiwa kusomewa maelezo hayo, Hakimu Lyamuya aliwaeleza kuwa hawatakiwi kuzungumza chochote kwa sababu mashtaka yanayowakabili ni ya uhujumu uchumi na pia shtaka la utakatishaji fedha halina dhamana.

Kuhusiana na suala la mawasiliano baina ya washtakiwa na ndugu zao, hakimu alisema “suala hili polisi wapo humu, wamelisikia watalishughulikia”.

Hakimu Lyamuya aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 22, mwaka huu itakapotajwa.

# Dk. Mwinyi asema majengo mapya Mji Mkongwe ni lazima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itaendelea kufanya uamuzi sahihi wenye faida kwa nchi, akisisitiza hayuko tayari kuona majengo ya Mji Mkongwe yanaanguka bila kujengwa mengine kwa faida ya nchi.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua shule ya kisasa ya Tumekuja baada ya ile ya awali iliyoko ndani ya Mji Mkongwe kubomolewa na kujengwa mpya katika eneo la Muembeladu, mjini Unguja.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuna baadhi ya watu wanatoka alichokiita ‘povu’ kwa kulalamika kuwa majengo hayo ya Mji Mkongwe yanatengenezwa.

Alisema lazima yatengenezwe kwa sababu mji huo ni urithi wa nchi, hivyo ni lazima vizazi vijavyo vifaidike.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa kabla ya ujenzi huo wa shule za kisasa, watoto walikuwa wanasoma katika shule zinazovuja maji wakati wa mvua na kukaa chini sakafuni wakiwa darasani.

Alisema wanafunzi walikuwa hawajui maabara, lakini sasa shule zote zina vifaa vya kisasa na hayo ndiyo maendeleo.

“Wale wanaosema ovyo, ninawaambia hadharani wala usingizi sikosi, nitaendelea kujenga shule za ghorofa mpaka watoto wetu wakae katika mazingira mazuri na darasa moja lisizidi wanafunzi 45,” alisema. Rais Dk. Mwinyi alisema uamuzi aliofanya wa kulitoa jengo la Shule ya Sekondari Tumekuja ni sahihi ambao kwa muda mfupi kumejengwa lingine ili wanafunzi waendelee na masomo yao.

“Kabla ya ujenzi wa shule hii, kulikuwa na mrundikano mkubwa wa wanafunzi darasani kwa darasa moja kuwa na wanafunzi 200 ambao walikuwa hawasomesheki,” alisema.

Rais Dk. Mwinyi alisema hivi sasa kunahitajika madarasa 5,000 ili wanafunzi waingie shuleni asubuhi kwa wakati mmoja na kuahidi ndani ya muda mfupi idadi hiyo ya madarasa itafikiwa.

Pia alipongeza walimu kwa kazi nzuri wanayofanya licha ya kipindi kirefu kuitekeleza katika mazingira magumu na kuahidi kuwa wakati wa kuwekewa mazingira mazuri umefika, wanafunzi watakuwa wachache darasani na shule kuwa na vifaa vya kisasa vya kufundishia.

Alisema shule hiyo itakuwa na uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 1,755 pamoja na kuwa na maabara za kisasa tatu na maktaba.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, alisema ujenzi wa shule hiyo umegharimu Sh. bilioni 4.4.

Mussa alisema tayari wizara imeanza kutumia mitaala mipya kwa wanafunzi wa shule za msingi, hatua ambayo itasaidia kuongeza kiwango cha ufaulu katika mitihani ya taifa.

“Mheshimiwa Rais Mwinyi niseme kwa ufupi kwamba, hivi karibuni tumetoa matokeo ya mitihani ya darasa la saba na darasa la nne na kuonesha kuwapo kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa michepuo pamoja na vipawa,” alisema.

Kamal

KAMAL GASES LIMITED

TAARIFA KWA UMMA

Sisi **Kamal Gases limited** wazalishaji namba moja wa gesi za viwandani zenye ubora uliothibitika na Shirika la viwango Tanzania TBS.

Tumegundua kuwepo kwa wazalishaji wa gesi wanaotumia mitungi yenye nembo ya KGL kinyume na sheria.

Tunawatangazia wazalishaji, watumiaji wa gesi za viwandani na umma kwa ujumla kwamba ni kinyume cha sheria kujaza, kuuza, na kusambaza gesi iliyowekwa kwenye mitungu yenye nembo ya kamal ambayo haikuzalishwa na Kamal Gases Limited.

Hivyo mnahabarishwa kwamba; Kamal Gases Limited wapo katika zoezi kabambe la kufuatilia na kukamata wahusika wote wanaozalisha gesi za viwandani na kujaza katika mitungi yenye nembo au alama ya kamal gases limited kinyume cha utaratibu.

Kamal Gases Limited itachukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufungua kesi za madai na jinai kwa yoyote atakaye tumia mitungi ya gesi yenye nembo ya Kamal Gases Limited kujaza gesi aliyoichakata mwenyewe au iliyochakatwa na wazalishaji wengine nje ya Kamal Gases Limited

Tunatoa wito kwa wateja wetu kuendelea kutumia huduma ya gesi ya Kamal Gases Limited kwa kupitia vituo vilivyoidhinishwa na kuitambulika na Kamal Gases Limited au wafike kiwandani chang'ombe industrial area plot no. 188/2 kwa maelezo zaidi piga simu namba **+255 765 169 444**

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Kamal Gases Limited**
**Dar es Salaam**

# Kilichojificha kuandika matusi kwenye mtihani

**Na Waandishi Wetu**

WATOTO walioandika matusi katika karatasi za majibu ya Mtihani wa Upimaji wa Kidato cha Pili na Darasa la IV mwaka 2023, wameibua mapya:

Viongozi wa dini wananyooshea kidole wazazi kuwa kiini cha tatizo; wataalamu wa saikolojia nao wanasema chanzo wazazi na jamii inayoendekeza lugha chafu mtaani.

Jumapili iliyopita, Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) lilitangaza matokeo ya Upimaji wa Taifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili Mwaka 2023, lilibainisha kuwa limefuta matokeo yote ya wanafunzi 17 kutokana na kuandika matusi kwenye karatasi za majibu.

Baadhi ya wadau waliozungumza na Nipashe jana kuhusu changamoto hiyo, walitaka maadili ya mtoto kwa ujumla yatazamwe.

Mzazi wa mtoto aliyefanya mtihani wa kidato cha pili mwaka jana na mkazi wa Dodoma, Joseph Kalimila, alisema kitendo hicho ni matokeo ya wazazi na walimu kutozungumza na wanafunzi kuhusu madhara ya vitendo hivyo.

Kalimila alisema ni lazima mzazi au mlezi ajiulize kama mtoto wake kabla ya kufanya mtihani huo, alimwonya kuhusu tabia za utovu wa nidhamu katika mitihani ikiwamo kuandika lugha za matusi.

"Binafsi nilimwambia 'ni heri usijaze chochote kuliko kuandika matusi'. Nilimweleza kuwa akiandika matusi au lugha yoyote isiyo na maadili, inaweza kumgharimu maisha yake yote na akaelewa," alisema Kalimila.

Blandina Yohana, mkazi wa Maili Mbili, mnada wa zamani jijini Dodoma pamoja na Sadik Msofe kutoka Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, walipendekeza wazazi wa watoto wanaoandika matusi katika mtihani, wachukuliwe hatua za kisheria kwa kile walichoeleza ni kutokana na kutokuwa karibu nao.

Mkazi wa Chona, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Shamira Doto, alisema huko vijijini kwao baadhi ya wazazi wamekuwa wanawataka watoto wao kuandika ovyo kwenye mitihani yao ya mwisho ili wasifaulu.

**VIONGOZI WA DINI**

Mwenyekiti wa Umoja wa Madhehebu ya Kikristo Mkoa wa Dodoma, Askofu Anthony Mlyashimba, alisema watoto kuandika matusi katika mitihani yao kwa sehemu kubwa kumechangiwa na baadhi ya wazazi kuwashawishi watoto hao wafanye vibaya katika mitihani.

Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary, alisema inasikitisha kuona vitendo hivyo katika kipindi ambacho serikali imewekeza mabilioni ya shilingi kwa ajili ya kuboresha elimu nchini.

Alisema kuwa wapo baadhi ya walezi na wazazi hawataki kushirikiana na watoto wao kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye masomo yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tanzania Early Childhood Education and Care (TECEC), Joel Elphas, alisema ubongo wa mtoto unaandaliwa akiwa tumboni, hivyo ni jukumu la serikali kuweka mkazo katika mpango wa malezi ya awali.

Elphas alisema serikali kupitia wa Mpango wa Taifa wa Programu Shirikishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto inatakiwa kuweka ufuatiliaji wa karibu kuanzia kwa mjamzito, mtoto anapozaliwa hadi kufikisha miaka minane na kuhakikisha mzazi anakuwa na mtoto wake wakati wote.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Mara, Neema Ibamba, alisema, "Ipo nafasi kubwa ya wadau wa maendeleo kushirikiana na serikali kutekeleza adhma hii ya kuwaelimisha wazazi na walimu kuhusu malezi bora."

Mtaalamu wa Elimu ya Awali na Utengenezaji wa Dhana za Kujifunzia kutoka TECEC, Ester Macha, alishauri wazazi watenge muda wa kukaa na mtoto hata kwa dakika 30 kwa siku ili kujua changamoto alizonazo pamoja na kumpa mafunzo ya vitu mbalimbali vinavyoweza kumjenga kiakili.

Kiongozi Shirikisho la Wamiliki wa Shule Binafsi Tanzania, Dk. Leonard Mao, alisema tatizo hilo linatokana na ufundishaji mbovu, hali inayosababisha mtoto kukosa majibu kipindi cha mtihani.

Dk. Mao alizishauri shule zote kuwajengea watoto msingi mzuri wa kuelewa tangu wakiwa madarasa ya awali ili wapate majibu ya kuandika katika mitihani yao.

**WASAIKOLOJIA TIBA**

Mtaalamu wa Saikolojia, Dismas Lyassa, alisema mama anapokuwa mjamzito na kupitia changamoto zitakazomsababishia msongo wa mawazo wa muda mrefu kama vile mimba kukataliwa au ugomvi wa kila mara huchangia wakati mwingine kuzaliwa mtoto akiwa hayupo sawa kisaikolojia.

Alitaja sababu ya pili ni mazingira aliyokulia mtoto na mambo aliyoshuhudia hasa katika umri wa mwaka mmoja hadi sita.

Alisema katika umri huo, mtoto anajifunza na kuweka vitu kichwani, hivyo kama alikulia katika mazingira ambayo waliomzunguka wanaongea matusi, hujifunza kwa kuweka kichwani na kuyatumia baadaye, hasa anapokuwa anapitia wakati mgumu.

"Mtoto wa aina hii hata mkimbadilisha vipi, ataonesha kubadilika, lakini inapofika wakati akapitia changamoto akashindwa kuitatua, kama vile kushindwa kupata majibu katika mtihani, kuna msukumo kichwani kwake unatokea na kumshawishi aandike lugha hiyo," alisema.

Katika mtihani huo, wanafunzi 206 wamefutiwa matokeo yao yote kutokana na udanganyifu waliofanya, wakiungana na wenzao 17 waliofutiwa kutokana na kuandika matusi.

*** Na Jenifer Gilla (DAR), Peter Mkwavila na Renatha Msungu (DODOMA), Vitus Audax (MWANZA), Shaban Njia (KAHAMA), Jaliwason Jasson (MANYARA) na Mary Mosha (MOSHI)**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**BODI YA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO TANZANIA**

Simu ya Upepo: *Kilimo"* DODOMA" Simu: +255(0) 26 2321192
Barua pepe: info@cpb.go.tz Tovuti: www.cpb.go.tz
Central Business Park, Eneo la Mbugani,
24 Barabara ya VETA, S.L.P. 337, DODOMA.

**10 Januari, 2024**

**TANGAZO LA UPANGISHWAJI WA GHALA JIJINI MWANZA.**

Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania (CPB), ilianzishwa ili kufanya biashara ya Mazao ya Nafaka na Mazao mengine mchanganyiko ili kuwa soko la uhakika kwa wakulima. Miongoni mwa majukumu ya Bodi hii, ni kushirikiana na wadau wengine katika utoaji wa huduma kama vile upangaji wa madaraja, ukodishaji wa maghala, huduma za uchakataji ili kuyaongezea thamani mazao na kuyauza katika masoko ya ndani na nje ya Nchi.

Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) inautangazia umma fursa ya upangishwaji wa Ghala No. 3, lililopo Kitalu No. 2A/2 mtaa wa Bohari Nyamagana, Mwanza. Ghala hilo lina ukubwa wa mita za mraba 1,625 kwa eneo la ndani ya ghala kwenye kiwanja chenye mita za mraba 6,000.

Wenye kutaka kupangisha wawasilishe maombi yao wakiainisha;

1. Majina kamili na anuani ya kudumu.
2. Aina ya Biashara anayotaka kufanya.
3. Ofa yake (*Biding price*).
4. Muda anaotaka kupangisha.
5. Nyaraka halali za usajili wa biashara kama vile leseni ya biashara, cheti cha mlipa kodi (Tax clearance) na nyaraka nyengine muhimu.

Maombi hayo yawe yamefika kwenye ofisi za CPB Makao Makuu kwenye anuani iliyooneshwa hapo juu kabla au ifikapo saa 9 Alasiri ya tarehe 20 Januari 2024.

Kwa mawasiliano Zaidi na fursa ya kukagua eneo husika tafadhali wasiliana nasi kwa barua pepe kupitia **info@cpb.go.tz** au nambari za simu **+255784 362 943.**

**WOTE MNAKARIBISHWA**

**Imetolewa na MKURUGENZI MKUU BODI YA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**

217780202

# Mkenda apiga marufuku michango lazima shuleni

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni siku tatu tangu kufunguliwa kwa shule, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amepiga marufuku shule kuweka michango ya lazima ambayo inawanyima watoto kuhudhuria masomo shuleni.

Prof. Mkenda alitangaza marufuku hiyo jana jijini hapa kwenye ziara ya ukaguzi wa ukamilishaji shule ya sekondari iliyoko Iyumbu, iliyojengwa na wizara hiyo.

"Ni marufuku kwa shule yoyote kuweka michango ya lazima ambayo mzazi au mtoto asipotoa mchango huo mtoto atakatazwa kwenda shuleni. Serikali imekamilisha utaratibu wa kutoa elimu bila ada mpaka kidato cha sita hatutarajii mzazi aambiwe atoe mchango wa lazima," alisema.

Aidha, aliwapongeza wazazi wanatoa michango yao kwa hiari na kusisitiza mtoto asirudishwe nyumbani kwa kutochangia dawati au chochote.

Akizungumzia matokeo ya mtihani wa darasa la nne na kidato cha pili, alionya shule ambazo zina tabia ya kuwaondoa wanafunzi ambao hawajafanya vizuri.

"Shule ambayo imekubali imepokea ada ya mtoto halafu inamwondoa mwanafunzi kwa kutofanya vizuri ili wabaki wenye akili, shule bora ni ile ambayo itakaa na kumwezesha mtoto afanye vizuri watakaoambiwa warudie watarudia lakini ukitaka kutuambia shule yako ni bora tumlete mtoto kwako tuoneshe na yule ambaye amesuasua ashikwe mkono twende naye," alisema.

"Tusichuje na kuwatenga watoto, sisi tutakuja kutafuta namna ya kupanga kuona mtoto aliingiaje na amemalizaje hiyo shule ndio ina haki ya kutembea kifua mbele, wazazi wanalalamika watoto wamefaulu lakini hawajafanya vizuri kufikia wastani wa shule basi wanaondolewa hili hatutaki kusikia," alisisitiza.

Kuhusu ukaguzi wa shule hiyo, alisema kwa sasa mchakato wa kutafuta jina unaendelea na itakuwa miongoni mwa shule zenye mkondo wa amali.

"Tunatarajia kufanya uzinduzi na tutakabidhi TAMISEMI na tumefurahishwa na ubunifu uliofanywa na SUMA JKT kwa kutengeneza gesi yao wenyewe kwa kutumia maji machafu ili kupunguza gharama za uendeshaji wa shule," alisema.

Hata hivyo, alisema mwaka ujao wa masomo wa kidato cha tano na sita itachukua wanafunzi wa tahsusi za sayansi kwa kuwa lengo la serikali ni kuzalisha wataalamu wengi wa sayansi watakaosaidia kada mbalimbali.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), Kanali Petro Ngata, aliishukuru serikali kwa kuliamini shirika hilo kutekeleza miradi mikubwa nchini na ujenzi wa mradi huo ulianza mwaka 2020 na hadi mwishoni mwa Januari, mwaka huu, utakuwa umekamilika.

# Mabilioni kujenga magati sita bandari za Dar, Bagamoyo

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetaja vipaumbele katika kuboresha ufanisi wa bandari, ukiwamo ujenzi wa magati sita yenye urefu wa mita 500 katika bandari za Dar es Salaam na Bagamoyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Placidus Mbossa, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kubainisha kuwa ujenzi huo utafanywa kwa njia ya ubia na sekta binafsi.

Alisema magati manne yatajengwa katika bandari ya Dar es Salaam na mawili bandari ya Bagamoyo na baada ya kukamilika yatasaidia kuongeza shehena.

Mbossa alisema gharama ya ujenzi wa gati moja ni Dola za Kimarekani kati ya milioni 100 hadi 150 ambazo ni gharama kubwa ndiyo maana wanapenda kufanyika kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).

Alitaja mikakati mingine ni ujenzi wa gati jipya la kuhudumia makasha, ujenzi wa eneo maalum la kuhudumia shehena zinazotoka au kwenda bandari ya Dar es Salaam na eneo la Kurasini.

Mikakati mingine ni usimikaji wa maboya mapya ya kupakulia mafuta, ujenzi wa bandari ya Bagamoyo na ujenzi wa matangi ya kupokelea na kuhifadhi mafuta.

Pia alisema kati ya Julai hadi Desemba, mwaka jana, TPA ilijiwekea lengo la kuhudumia meli 792 ambazo hadi kumalizika kwa muda huo, ilihudumia meli 979 sawa na asilimia 123 ya lengo.

Alisema kwa meli kubwa zilizohudumiwa, TPA ilikuwa na lengo la kuhudumia tani 15,576,000 katika kipindi cha Julai hadi Desemba, mwaka jana, na ilivuuka lengo na kufikia tani 17,200,692 sawa na asilimia 110.4.

"TPA ilikuwa na lengo la kuhudumia tani 10,993,000 katika bandari ya Dar es Salaam na hadi kufikia Desemba , 2023 ilikuwa imehudumia tani 12,052,682 ambazo ni sawa na asilimia 109.6 ya lengo," alisema Mbossa.

Julai hadi Desemba, 2023 alisema TPA ilihudumia makontena 509,594 ambazy ni sawa asilimia 102.8 za lengo lililowekwa la kuhudumia makontena 495,600 katika kipindi hicho.

Alisema watu waliohudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam hadi Desemba mwaka jana walikuwa abiria 987,228 sawa na asilimia 98.3 ya lengo lililowekwa katika kipindi cha Julai hadi Desemba kufikia abiria 1,004,167.

Aidha, alisema TPA inaendelea kuhudumia meli na shehena katika mwaka wa fedha 2023/24 kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya meli na shehena katika bandari ya Dar es Salaam.

Ongezeko hilo, alisema ni matokeo ya mikakati ya maboresho ya huduma za bandari ili kuongeza tija na ufanisi.

Alisema wametoa tozo shindani zinazoendana na hali ya soko na mahitaji ya mteja mmoja mmoja. Mamlaka imekuwa ikipitia tozo zake mara kwa mara kwa kushirikiana na wadau katikakuhakikisha Mamlaka inakuwa na tozo shindani.

Kwa mujibu wa Mbossa, kuanza kwa matumizi ya bandari kavu ya Kwala kwa lengo la kuwavutia wateja wa bandari kwa kuongeza muda huru hadi siku 30 kwa makasha ya ndani na siku 60 kwa makasha ya jirani.

Mbossa alitaja sababu zingine za kuongezeka kwa meli ni kuboresha huduma kwa wateja, kufanya kampeni kimasoko na kuonana ana kwa ana na wateja wa ndani na nje ya nchi, kuimarisha ofisi za kimasoko zilizoko nje ya nchi na kufungua mpya, ushirikiano na wateja na wadau wa bandari.

Aidha, alisema changamoto iliyoko katika bandari ya Dar es Salaam ni uchache wa magati kwa kuwa yaliyopo ni 12 yaliyotengwa kwa ajili ya kuhudumia shehena za magari, kichele, makasha na mizigo mchanganyiko.

"Kwa hiyo miundombinu ya gati iliyopo bandarini ina uwezo wa kuhudumia jumla ya meli zisizozidi 12 kwa wakati mmoja," alisema.

Mbossa alisema licha ya maboresho yaliyofanywa katika bandari ya Dar es Salaam kupitia mradi wa DMGP awamu ya kwanza, changamoto ya uchache wa idadi ya magati na vitendelea kazi imeendelea kuathiri utendaji kazi wa bandari hiyo.

"Tatizo huwa kubwa zaidi na kuonekana kipindi cha msimu mkubwa wa shughuli za bandari ambacho huanza Septemba hadi mwanzoni mwa Februari kila mwaka," alisema,"alisema

Alisema miundombinu ya reli haijitoshelezi na barabara ambayo ingesaidia kurahisisha uondoshaji wa shehena bandarini kwa haraka.

Mbossa alisema changamoto ya kuharibka mara kwa mara kwa mitambo ya kuhudumia shehena kutokana na uchakavu wa mitambo, hivyo kusababisha kushuka kwa tija na kuchagiza kuchelewa kutoka kwa meli katika magati.

Aidha, alisema tatizo jingine ni kuongezeka kwa meli kubwa kulinganisha na uwezo wa bandari kuanzia Oktoba hadi Dsemba 2023. Ongezeko hilo limesababisha msongamano wa meli nyingi kusubiri nje ya bandari kwa wastani wa siku 10 na kusababisha malalamiko kutoka kwa wateja.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa Oktoba mwaka jana bandari ya Dar es Salaam ilihudumia kiwango kikubwa cha meli 101 na bado kulikuwa na meli 32 zilizosubiri nje ya bandari kuhudumiwa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

*Dar es salaam Januari 10, 2024*

**TAARIFA KWA UMMA**

**TEMBELEA TOVUTI YA NIDA KUFAHAMU KITAMBULISHO CHAKO KILIPO**

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inapenda kuwafahamisha wananchi kuwa vitambulisho vya Taifa vimechapishwa na kusambazwa maeneo mbalimbali. Kadhalka, orodha ya majina ya watu wote ambao vitambulisho vyao vimechapishwa imewekwa kwenye tovuti ya Mamlaka kupitia kiunganshi **https://vitambulisho.nida.go.tz**

Hivyo, mwananchi ambaye hujachukua kitambulisho chako, unaweza kufahamu kwa kupitia tovuti hii Ofisi ya serikali ya Mtaa/Kijiji ambapo kitambulisho chako kipo kwa ajili ya kukichukua. Aidha, unaweza kutembelea tovuti ya Mamlaka kupitia **www.nida.go.tz** kisha bofya mahali palipoandikwa **Kitambulisho cha Taifa ikifuatiwa na Fahamu Kitambulisho kilipo**. Baada ya hapo ukurasa unaoonyesha mikoa utafunguka, Chagua mkoa na kufuatiwa na wilaya uliyojisajili na baadae bonyeza Kata ikifuatiwa na Kijiji/Mtaa uliokuwa unaishi wakati unajisajili. Baada ya hapo ukurasa wenye orodha ya majina na mahali Kitambulisho chako kilipo utafunguka.

Ukiona jina lako tafadhali nenda kachukue Kitambulisho chako mahali kilipo mapema kwani baada ya mwezi mmoja kupita vitarejeshwa ofisi za NIDA za wilaya, hivyo utalazimika kukifuata katika ofisi ya NIDA ya Wilaya uliyojisajili.

Usomapo au kusikia tangazo hili tafadhali mjulishe na mwingine

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Mawasiliano**
**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

**Barabara ya Kilimani, S.L.P 12324, Dar es Salaam, Simu: +255734220962,**
**Barua pepe: info@nida.go.tz, Tovuti: www.nida.go.tz**

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni jambo jema kuwathamini watu wenye ulemavu Z'bar

**WATU** wenye ulemavu Zanzibar wamewekewa mazingira mazuri ya kujisomea ikiwa ni miongoni mwa fikra za waasisi wa Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 ambayo ni kuwapatia elimu iliyo bora wananchi wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Kitendo hicho ni cha kupongezwa kwa kuwa mara nyingi watu wenye ulemavu husahaulika na kupata changamoto nyingi katika maisha yao ya kila siku.

Katika kuadhimisha Miaka 60 ya Mapinduzi, Serikali ya Zanzibar imefungua Kituo cha Elimu Mjumuisho kilichoko Pujini, Wilaya ya Chakechake Pemba ikiwa ni mwendelezo wa shamrashamra za maadhimisho ya sherehe hiyo.

Zanzibar inatekeleza mipango ya kitaifa na kimataifa kwa kuhakikisha shule za Elimu Mjumuisho zinakuwa na huduma bora zitakazowawezesha wanafunzi kupata elimu wezeshi na kujenga jamii yenye usawa na inayowajali watu wote.

Utekelezaji wa elimu hiyo ni katika hatua za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Kitaifa wa Zanzibar (ZAPED 2021-2026) na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG - 2030) ambao kwa pamoja inasisitiza suala la utoaji wa Elimu Mjumuisho kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Suala kubwa linalosisitizwa ni wananchi kutoa ushirikiano wao katika kuwaandikisha vijana wao katika shule maalumu ili kuwapa fursa ya kupata haki yao ya msingi ya kujisomea kama wanavyosoma watoto wengine.

Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Mwinyi imewapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwa kuzingatia uwapo wao katika kila miundombinu inayojengwa na serikali ili waweze kushiriki katika mambo yote ya maendeleo.


Wananchi hasa wa Pujini na vijiji jirani wana wajibu wa kutoa ushirikiano kwa walimu na viongozi wa shule hiyo maalum katika kuitunza vyema miundombinu hiyo na kuilinda ili iweze kudumu kwa muda mrefu na walimu kuwa na mapenzi na imani kubwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu hasa kwa vile wanahitaji uangalizi wa hali ya juu katika ufundishwaji wao.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, ameeleza umuhimu wa Kituo cha Elimu Mjumuisho unaotokana na ongezeko la wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambao walikuwa wakikosa shule zinazoendana na uhitaji wao na wengi wao kubaki majumbani hali iliyokuwa ikiwakosesha haki yao ya msingi ya kupata elimu bora.

Kukamilika kwa kituo hicho kumekidhi viwango vinavyoendana na maadhimisho ya kimataifa yanayoelekeza watu wenye mahitaji maalum kupatiwa elimu kulingana na uhitaji wao ikiwa ni pamoja na walimu wenye uwezo, vifaa na vitendea kazi vya kusomea na kusomeshea watu wenye mahitaji maalum.

Kana anavyoeleza Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdulla Said, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inaelekeza watoto wote kupatiwa haki sawa bila ya kujali tofauti zao jambo linalofanya Serikali ya Awamu ya Nane kulipa kipaumbele suala la ujenzi wa shule za elimu Mjumuisho.

Ujenzi wake ambao umekamilika kwa kiwango cha hali ya juu wenye majengo saba, kuna vyumba vya kusomea, madahalia kwa wanafunzi wa kike na wa kiume pamoja maabara na umegharimu zaidi ya shilingi bilioni nne.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Kujiongeza kunamaliza kilio ugumu wa maisha

**MWAKA** unavyoanza watu hujiongezea malalamiko maisha magumu. Ni sauti zinazosikika mijini na vijijini, lakini kuna mengi ya kujaribu ili maisha yasonge.

Kikubwa ni ubunifu katika maisha kwa vile ni muhimu hasa kwa sababu ndiko zinakotoka chachu za maendeleleo zinazochagiza nini kifanyike ili kusonga mbele zaidi na kuwa na maisha bora.

Kuna mambo mengi yanafanyika hasa kwenye ujasiriamali na utafutaji lakini bila ubunifu inawezekana kusiwe na tija, mfano kufuga kuku unapojikita kwenye eneo hili ni lazima ujue unafuga aina gani ya kuku, wanakula chakula gani , kuonana na wataalamu na pia kuongeza mbinu ili uibuke na mafanikio.

Mathalani mijini chakula pendwa hasa na vijana iwe shuleni, mitaani, kazini, nyumbani ni chipsi yai au kuku, fikiria ni mayai kiasi gani yatahitajika mijini na majijini kulisha mamilioni ya wateja?

Ni mambo yanayokupa hamasa, kujaribu kufuga ili kujikomboa kiuchumi , badala ya kulalamika maisha ni magumu.

Siyo kuku tu kuna ufugaji wa ng'ombe na mbuzi halikadhalika kondoo usiache kwenda kwa wataalamu wa afya ya mifugo ili kukupa ushauri kuhusu ufugaji na pia pekua mitandao zungumza na wasomi wa kilimo na ufugaji ili ujiongeze hasa kwenye lishe na kupata nyama na maziwa bora.

Kujiongeza na ubunifu kwa kijana wa kiume au wa kike kunakupeleka kwenye kuuza maua. Angalia vionjo gani mjasiriamali kwenye kuuza maua vinaweza kukutoa. Buni mbinu kama kuweka maua kwenye plastiki zinazofanana na vioo ili kuyapa mvuto zaidi.

Tafuta virutubisho vinavyoweza kuzipa waridi muda mrefu zaidi wa kuishi ili mteja anaponunua akae nazo kwa siku nyingi kuliko ilivyo sasa.

Unaweza kujinyanyua kiuchumi kwa mbinu nyingi zinazohusisha ubunifu na kutafuta maeneo mazuri ambayo utaotesha maua yenye kuvutia na kujipatia wateja wazawa kwa wageni kwani bidhaa hiyo inapendwa na wengi hivyo una weza kuendesha gurudumu la maisha bila 'stress'.

Maisha yanaweza kwenda na kufanikiwa kwenye ufugaji wa samaki anza kupata ushauri kuhusu ufugaji huo tafuta wataalamu wanao shughulika na mifugo hiyo ili kutambua aina za vyakula na mazingira bora ili kufikia kwenye malengo unayoyatamani.

Kumbuka maelfu wanashauriwa kuacha nyama na kula samaki ni fursa kwa vile hii ni nyama nyeupe isiyo na madhara kama zilivyo nyama nyekundu za ng'ombe na mbuzi.

Wakati huu ni wa kukumbuka kuwa kilimo ni muhimu sana kwani hii ndiyo sehemu pekee ambayo mtu anapata chakula na ndiyo uhai na msingi ni jambo muhimu.

Vijana kwa watu wazima kilimo cha kisasa cha mboga na matunda kina manufaa na kuna wakati watu wanaiita kazi ya Eden au ya Muumba kwa vile maandiko yanasema wa kwanza kulima ni Mungu, aliyeandaa bustani ya Eden na kuweka mazao yote yanayoonekana duniani leo.

Mboga kuanzia mchicha, tembele, maboga, spinachi za aina zote ni chakula kinacholiwa mjini kila siku . Ni mlo rahisi na aghalabu kila nyumba unapatikana kwanini Watanzania wasipende kilimo?

Tengeneza sabuni za maji za aina mbalimbali lakini angalia kitu gani kinakosekana kwenye bidhaa hizo sokoni sasa.

Ukiingia kwenye ujasiriamali huu kuwa mbunifu zalisha sabuni za maji za watu kwa mfano wanaoishi kwenye mazingira ambayo hayana maji ya baridi.

Jijini Dar es Salaam na miji mingine kuna sehemu zinazotumia maji chumvi ya kuchimba kwenye visima. Hawa ni wateja wako watengenezee sabuni za kuogea na kufulia kwenye maji yenye chumvi.

Ukipita madukani kuna sabuni za maji za kuogea zalisha sabuni bora zisizo na mzio au aleji kwa ajili ya watoto wadogo, lakini pia za kufulia nguo nyeupe pekee , au za kufulia vitenge na uhakikishe kuwa unakuwa na bidhaa zenye ubora na uhalisia wa kile unachozungumza au kutangazia wateja.

Furahia mwaka mpya kwa kujituma na kuwa mbunifu siyo kuendelea kulalamika mambo magumu bila kuchukua hatua.

HABARI KITAIFA

# Wakulima mikoa sita wafikiwa mradi wa kuwajengea uwezo

**Na Godfrey Mushi,**
MOSHI

MRADI wa kujenga uwezo unaohusiana na Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira (ACP MEAs III), umepata matokeo chanya baada ya kufanikiwa kuwasaidia wakulima katika mikoa sita nchini.

Mikoa hiyo ni Dar es Salaam (Kigamboni), Morogoro (Kilosa), Iringa (Kilolo), Mbeya (Mbarali), Arusha (Karatu) na Kilimanjaro (Same) ambako mradi huo umewasaidia wakulima kutumia mbinu mbalimbali za kilimo na kupunguza matumizi makubwa ya kemikali za mbolea.

Mradi huo ambao unatekelezwa na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), pia umekuja na majibu ya kina kwanini baionuai nyingi zinapotea.

Sehemu ya utafiti inaonesha baionuai hiyo hupotea kupitia kilimo kutokana na matumizi ya kemikali za mbolea ambazo wakulima hutumia bila kuwa na uelewa wa kutosha au kutumia kemikali zilizokwisha muda wa matumizi.

Akizungumza jana katika mafunzo ya siku sita yaliyoanza juzi katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Mratibu wa Mradi huo (NPC-FAO), Diomedes Kalisa, alisema lengo kubwa ni kuangalia ni kwa namna gani baionuai ambazo zimeanza kupotea, zinaweza kuhuishwa.

Kalisa alisema mradi huo ambao unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), ulianzishwa mwaka 2019 na utafikia ukomo wake mwaka huu, ukitekelezwa katika mabara matatu ya Afrika, Caribbean na Pasifiki.

"Kuna shughuli mbalimbali ambazo zimefanyika, ikiwamo namna ya kusaidia wakulima kutambua mbinu mbalimbali ambazo zinafaa wakati wanafanya shughuli zao za kilimo katika urutubishaji udongo.

"Wamenufaika na mafunzo ya kupunguza matumizi makubwa ya kemikali za mbolea, ili kurudisha udongo katika ule uhalisia wake.

"Wanawezeshwa pia kutambua magonjwa kwenye mifugo. Yale ambayo yanasabisha pia upotevu wa baionuai katika maeneo ya mifugo. Maofisa mifugo wamefundishwa katika wilaya zote, na wamefundishwa mfumo wa kuangalia haya magonjwa na kutoa taarifa kwa wizara zinazohusika," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi Mkuu wa TPHPA, Prof. Joseph Ndunguru, alisema yanahusisha wakaguzi 32 wa viuatilifu kutoka kwenye mipaka yote, maduka na maeneo mbalimbali, ambako matumizi au utengenezaji viuatilifu unafanyika.

Prof. Ndunguru alisema utoaji mafunzo hayo unalenga kuwajengea uwezo wataalamu ili wafanye kazi za ukaguzi wa viuatilifu.

"Lengo kuu ni kwamba unapokuwa na ukaguzi wa viuatilifu, maana yake unachangia ule mkakati wetu wa kuwa na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu, ili kulinda afya ya binadamu na mazingira.

"Tunaendesha haya mafunzo TPHPA kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo ambao ni FAO na EU, ambao wamechangia katika kutoa fedha za kuendeshea mafunzo haya," alisema.

Prof. Ndunguru alisema faida kubwa ambayo itatokana na mafunzo hayo ni kuongezeka tija katika mazao ya kuboresha masoko ya mazao kwa kuwa na mazao yenye kiwango kikubwa cha ubora ambacho kitauzwa nje na kuliingizia taifa fedha za kigeni.

Alisema wanakwenda kupunguza visumbufu vya mimea kwa maana ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao na kuwapo viuatilifu bandia sokoni.



Baadhi ya viongozi wa kimila wa kabila la Wabarbaig pamoja na baadhi ya viongozi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki wakisaini mkataba wa kuchepusha bomba la mafuta linalopita katika kijiji cha Gorimba, Wilaya ya Hanang' jana ili kukwepa kaburi la mmoja wa viongozi wa kimila wa kabila hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi wa Butimba kutatua kero ya maji mkoani Mwanza

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, ameihakikishia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuwa kero ya maji ya muda mrefu iliyoko mkoani mwake itakuwa historia baada ya kukamilika mradi mkubwa wa maji wa Butimba.

Akizungumza na wajumbe wa kamati hiyo ofisini kwake jana jijini, Mkuu wa Mkoa alisema mradi huo umefikia asilimia 100 ya utekelezaji, ukitarajiwa kutoa lita milioni 148 kwa siku.

"Mradi huu sasa utawanufaisha wakazi wa Nyamagana, Ilemela, Misungwi na Magu. Tunaipongeza sana kamati hii kwa usimamizi mzuri wa fedha hizi za bajeti zinazotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi," alisema Makalla.

Mkuu wa Mkoa alitaja miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa mkoani mwake kuwa ni pamoja na ukarabati wa uwanja wa ndege unaotarajiwa kuanza mwezi ujao na kukamilika mwezi Juni, mwaka huu ambapo pamoja na mambo mengine, utasaidia kusafirisha mizigo ya minofu ya samaki kutoka Mwanza kwenda Nairobi.

"Tayari tumefanya mazungumzo na uongozi wa ATCL (Kampuni ya Ndege Tanzania) kuhusiana na usafirishaji mizigo hiyo baada ya kupata usumbufu wa kwenda kuisafirisha mbali na uwanja wetu wa Mwanza upo," alisema Makalla.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Daniel Sillo, alisema kamati yake imezuru Mwanza ikiwa ni sehemu ya majukumu yake ya kukagua miradi yote inayotekelezwa kwa fedha za serikali ili kujionea maendeleo na changamoto zake na baadaye kutoa ushauri serikalini.

"Tuna kazi ya kuhakikisha mipango yote ya maendeleo ya kiuchumi nchini inatekelezeka kama ilivyokusudiwa. Tupo Mwanza kukagua mradi wa chanzo cha maji Butimba.

"Rais amekuwa mstari wa mbele kutafuta fedha na serikali yake kuzitoa kwa maendeleo ya wananchi, hivyo ni wajibu wetu kuhakikisha tunamuunga mkono kwa kusimamia ipasavyo," alisema Sillo.

# Hospitali ya Tumbi yatakiwa kuimarisha dawati la maoni

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Jingu ameagiza Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani (Tumbi) kuimarisha njia za kupata mrejesho kutoka kwa wanaowahudumia.

Ametaka kuwapo mfumo rasmi utakaojulikana kwa kila anayefika kupata huduma hospitalini huko ili kutoa maoni sambamba na kuimarisha dawati la upokeaji maoni ambalo litakuwa sehemu ya wazi.

Alitoa maelekezo hayo jana mjini hapa baada ya kutembelea hospitalini huko na kuzungumza na wagonjwa waliokuwapo wodini na baadaye baadhi ya watumishi, huku akisisitiza utoaji huduma bora za afya.

Dk. Jingu alisema kila wakati kunatakiwa kuwa na mtu au watu wa kupokea maoni na kusisitiza kuwa jambo hilo ni muhimu kwa hospitali zote za rufani na linapaswa kufanyika kwa faragha ili kila mtu atoe maoni yake bila wasiwasi. "Tukipata mrejesho kutoka kwa wale tunaowahudumia, basi tutajua ni namna gani tunaweza kuboresha huduma zetu ambazo ni nzuri ili kuwa nzuri zaidi," alisema.

Kiongozi huyo pia alisema ni lazima watoahuduma waimarishe mawasiliano na watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali ikiwamo kuzungumza.

Alisema hospitali inatakiwa kuteua watu kwenda kupata mafunzo ili kuwa na ujuzi wa kuhudumia kundi hilo pindi wanapofika kupata huduma za kiafya.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, aliwataka watumishi wa afya kuhakikisha wanazingatia miiko ya kazi na maadili wakati wa kutoa huduma.

Prof. Nagu alisema wakati wa kutoa huduma hizo ni lazima wataalamu wa afya kuzingatia taratibu za kujikinga kabla hawajaanza kuhudumia mgonjwa ili kuepuka kuhatarisha afya zao.

# WHI yatakiwa kubuni nyumba za watumishi wa umma

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameitaka Taasisi ya Watumishi Housing Investments (WHI) kuja na ubunifu wa kujenga makazi bora ya watumishi wa umma katika maeneo ya mijini jirani na maeneo ya shule na hospitali ili kuwaondolea changamoto ya makazi manesi na walimu na kuboresha utendaji kazi wao.

Amesema maeneo ya mijini, shule pamoja na hospitali zinamiliki maeneo makubwa ambayo Taasisi ya WHI inaweza kuyatumia kujenga majengo marefu kwenda juu ili kuwafanya walimu na manesi wafurahie kutoa huduma kwa wananchi kwa kuishi kwenye makazi bora jirani na maeneo ya kazi.

Simbachawene alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na timu ya menejimenti ya WHI ikiwa ni mwendelezo wa kusikiliza changamoto zinazoikabili taasisi anazozisimamia pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa wakati wa ziara aliyoifanya mwezi Agosti, mwaka jana. Alisema katika maeneo ya mijini watumishi wakiwamo walimu na manesi wanalazimika kutafuta makazi mbali na maeneo wanakofanyia kazi kwa vile ni vigumu kupata nyumba na hata zikipatikana gharama zake ni kubwa kulingana na kipato chao.

"Hakuna asiyejua umuhimu wa walimu na manesi katika nchi hii, lakini wengi wamekuwa wakiishi maeneo ya mbali na wanakofanyia kazi na kulazimika kulipa nauli kubwa kwa vile hawawezi kumudu kulipa kodi ya makazi yaliyo jirani na maeneo yao ya kazi, waguseni hawa kwa kuwajengea makazi bora," alisema.

Alisisitiza kuwa nyumba zikiwa jirani na eneo la kazi inasaidia kupunguza gharama za maisha na kuongeza ufanisi kazini na hilo ndio lengo la serikali kuhakikisha watumishi wanafurahia mazingira ya kazi kwa gharama rafiki.

Alisema watumishi wa umma wakiwamo walimu na manesi wanaofanya kazi katika maeneo ya mijini wanalazimika kusafiri umbali mrefu kutokana na changamoto ya makazi na kusababisha kutoa huduma zisizoridhisha kwa wateja wao.

Kadhalika, kitendo cha watumishi wa umma kutokuwa na makazi bora na kuwa mbali na maeneo yao ya kazi ni changamoto kubwa inayoathiri utendaji kazi na kuitaka taasisi hiyo kuona umuhimu wa kufanya hivyo kwa kuwa ni utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020/ 2025.

Alisema ujenzi wa makazi bora karibu na maeneo ya kazi, utawasaidia watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza kutohangaika.

"Mkijenga nyumba maeneo ya jirani na vituo vya kazi, kutawasaidia sana watumishi kutoichukia kazi kwa kuwa watapata sehemu nzuri ya kuishi," alisisitiza.

Mkurugezi wa Taasisi ya Watumishi Housing, Dk. Fred Msemwa, alisema kwa mwaka 2023/24 imeendelea na ujenzi wa nyumba Njedengwa, Magomeni na Gezaulole ili kupunguza adha wanazozipata watumishi wa umma wakiwamo walimu na manesi.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Simon Maigwa (wa tatu kulia), akikabidhiwa funguo za pikipiki nne mwishoni mwa wiki na Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo (wa tatu kushoto), alizozitoa kwa jeshi hilo ili kusaidia kufanya doria mkoani humo. **PICHA: JAMES LANKA**

# Waziri aagiza kufunguliwa barabara Katavi - Songwe

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, ameutaka Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), kufungua mawasiliano ya barabara kutoka Katavi kwenda Songwe kupitia Bonde la Mto Rukwa.

Kasekenya alisema hayo juzi wakati akikagua daraja hilo ambalo limeathiriwa na mvua inayoendelea kunyesha na kusababisha kukatika kwa mawasiliano kati ya mikoa hiyo.

"Niwaagize TANROADS kuhakikisha kazi inaendelea kwa kasi bila kusimama na mawasiliano yanarudi kama ilivyokuwa hapo awali, maana daraja hili ni muhimu kwa wananchi wa kata ya Mtowisa na Zimba, Mkoa wa Rukwa wote kwa ujumla na Mkoa wa Songwe," alisema Kasekenya.

Aliwataka wananchi kutunza miundombinu ya barabara pamoja na kuacha kuharibu vyanzo vya maji huku akiwataka TANROADS na uongozi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara kutembelea miundombinu ya barabara mara kwa mara hususani katika kipindi hiki cha mvua. Meneja wa wakala huyo Mkoa wa Rukwa, Mgeni Mwanga, alisema timu ya wataalamu inafanya kazi usiku na mchana kurejesha mawasiliano ya daraja hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Nyakia Ally alisema mvua kubwa iliyonyesha katika wilaya hiyo imesababisha madhara kwenye mashamba, nyumba, barabara pamoja na madaraja na kuwashukuru TANROADS kwa kuanza kazi ya kurejesha miundombinu ya daraja hilo katika hali ya kawaida.

"Tunaishukuru kupitia Wizara ya Ujenzi na TANROADS kwa kutujengea daraja la muda tukiwa tunasubiria kurejeshewa daraja la awali ambalo mawasiliano yake yamekatika. Kurejeshwa kwa daraja la Mto Rukwa ambalo linaunganisha Mkoa wa Rukwa, Katavi na Songwe kutaimarisha uchumi, biashara na uwekezaji wa wananchi katika mikoa hiyo," alisema Nyakia.

# Wenye ulemavu wapewa kipaumbele elimu kuenzi waasisi wa Mapinduzi

**Na Suleiman Omar**

SERIKALI imewapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kujisomea ikiwa ni miongoni mwa fikra za waasisi wa Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 ambayo ni kuwapatia elimu iliyo bora wananchi wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Hayo yamesemwa na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, wakati wa ufunguzi wa kituo cha elimu Mjumuisho kilichopo Pujini, Wilaya ya Chake Chake, Pemba, ikiwa ni mwendelezo wa shamra shamra za kutimiza miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema kuwa Zanzibar inatekeleza mipango ya kitaifa na kimataifa kwa kuhakikisha shule za elimu Mjumuisho zinakuwa na huduma bora zitakazowawezesha wanafunzi kupata elimu wezeshi na kujenga jamii yenye usawa na inayowajali watu wote.

Suleiman alisema utekelezaji wa Elimu Mjumuisho ni katika hatua za Mpango wa Maendeleo ya Kitaifa wa Zanzibar (ZAPED 2021-2026) na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG 2030) ambayo kwa pamoja inasisitiza suala la utoaji wa elimu Mjumuisho kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Aidha, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano wakati wa kuwaandikisha vijana wao katika shule hiyo ili kuwapa fursa ya kupata haki yao ya msingi ya kujisomea kama watoto wengine.

Alisema Serikali ya Awamu ya Nane imewapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwa kuzingatia uwapo wao katika kila miundombinu inayojengwa na serikalini ili waweze kushiriki katika mambo yote ya maendeleo.

Aliwataka wananchi wa Pujini na vijiji jirani kutoa ushirikiano kwa walimu na viongozi wa shule hiyo kuitunza vyema miundombinu hiyo na kuilinda ili iweze kudumu kwa muda mrefu na kuwataka walimu kuwa na mapenzi na imani kubwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu hasa kwa vile wanahitaji uangalizi wa hali ya juu katika ufundishwaji wao.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, amesema uzinduzi wa Kituo cha Elimu Mjumuisho, unatokana na ongezeko la wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambao walikuwa wakikosa shule zinazoendana na uhitaji wao na wengi wao kubaki majumbani jambo linalowakosesha haki yao ya msingi ya kupata elimu bora.

Lela alisema shule ya Elimu Mjumuisho Pujini imekamilika ikiwa imekidhi viwango vinavyoendana na maadhimio ya kimataifa yanayoelekeza watu wenye mahitaji maalum kupatiwa elimu kulingana na uhitaji wao ikiwa ni pamoja na walimu wenye uwezo, vifaa na vitendea kazi vya kusomea na kusomeshea watu wenye mahitaji maalum.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdulla Said, amesema Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza watoto wote kupatiwa haki sawa bila ya kujali tofauti zao.



# Mil. 242/- zaboresha miundombinu elimu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI Kuu imetoa Sh.milioni 242 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu ikiwamo kujenga vyumba vipya vya madarasa katika Shule ya Msingi ya Murieti Darajani iliyoko Kata ya Sokoni One katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Taarifa ya kutolewa kwa fedha hizo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Arusha,John Mongela,wakati akizungumza wazazi na walezi waliojitokeza kuwaandikisha watoto wao darasa la awali na la kwanza katika Shule ya Msingi Murieti Darajani.

"Wiki hii imeshaletwa Sh.milioni 242 ambazo tayari zimeshawekwa kwenye akaunti ya shule ni maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan baada ya kupitia orodha za shule na kuona hali ilivyokuwa,"alisema Mongela.

Kadhalika ameagiza Halmashauri ya Jiji la Arusha kuanza utaratibu wa kujenga shule mpya ya msingi katika Kata ya Sokoni One kwa kuwa hata kukiongezwa majengo mengine ya ghorofa bado shule itakuwa na idadi kubwa ya wanafunzi.

"Walimu 65 walioko hawatoshi kwa kuwa hapa tuna wanafunzi 4900 hivyo tunapaswa kuwapongeza na kuwatia moyo walimu wetu kwa kuwa wanafanya kazi kubwa,"alisema Mongela.

Licha ya kuzungumza hayo,aliwataka wazazi kutokuwategemea walimu peke yao kwa kuwa na wao wana jukumu la kuwajibika katika malezi ya watoto ikiwamo kuwapatia mahitaji muhimu.

"Serikali chini ya uongozi wa Rais Samia inahangaika kuwekeza kwenye elimu kuhakiki kila mtoto anapata elimu na kwa watoto wetu na hawa ndio ambao tuwatapata wakuu wa mikoa, mawaziri na viongozi wengine hivyo rai yangu kwa wazazi na walezi timizeni wajibu wenu ikiwamo kuhakikisha watoto wanakuja shuleni,"aliongeza.



Mkuu wa Wilaya ya Hanang' Janeth Mayanja (katikati) akipokea sare za shule na vifaa vya kusomea kutoka kwa Katibu wa Afya Mkoani Manyara, Thomas Malle (wapili kushoto) vilivyotolewa na chama cha makatibu wa afya Tanzania (AHSATA) kwa wanafunzi walioathirika na maafa ya mafuriko Hanang' juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC anusa upigaji ujenzi wa shule

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(TAKUKURU), kuchunguza mradi wa ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Murieti Mlimani iliyoko Halmashauri ya Jiji la Arusha, kwa madai kuwa kuna harufu ya upigaji wa fedha za serikali.

Mkuu huyo wa Mkoa ametoa agizo hilo jana,jijini hapa wakati wa ziara ya kikazi kukagua uandikishaji na upokeaji wa wanafunzi wanaotakiwa kujiunga na darasa la kwanza, awali na kidato cha kwanza.

Mongela pia aliwaonya viongozi wa jiji hilo wasijaribu kutumia fedha zinazotolewa kwa ajili ukarabati kwenye shule za msingi na sekondari kwa maslahi yao binafsi.

Kadhalika ameagiza Jiji hilo, kuongeza umakini kwenye usimamizi wa miradi ya maendeleo ili iendane na thamani halisi ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

"Rai yangu hapa Jiji la Arusha umakini uongezeke kwa kuwa hatuwezi kuvumilia hii hasara na sijui kama mnanielewa na huo ndio ujumbe wangu," alisema Mongela.

"Haiwezekani halmashauri nyingine za mkoa huu, zinazopewa fedha sawa na Jiji la Arusha zinatekeleza miradi kwa wakati na kwa viwango vya hali ya juu ikilinganishwa na thamani halisi ya fedha lakini nyie Jiji ambao mnakusanya mapato mengi mmekuwa wababaishaji," alisema Mongela.

Alitoa mfano wa Ngorongoro ambapo ubora wa kazi yao upo juu ukilinganisha na wilaya hiyo licha ya gharama za kupeleka vifaa vya ujenzi ikiwamo mifuko ya saruji kuwa juu.

"Kwa nini wanamaliza kazi kwa muda kuliko Jiji la Arusha ambao vitu vyote vinapatikana hapa na kutoka hapa kupelekwa kwenye halmashauri za Ngorongoro, Longido na Karatu ambazo ziko pembezoni mwaka mkoa huu na ubora wao uko juu kuliko nyie, alihoji Mongela."

# DC aagiza wanafunzi kuhudhuria masomo

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk.Suleiman Serera, amewaagiza maofisa watendaji wa kata, kuhakikisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wanahudhuria masomo baada ya shule kufunguliwa.

Dk. Serera aliyasema hayo baada ya kutembelea shule mbalimbali za msingi na sekondari, kukagua mahudhurio ya wanafunzi, ikiwa ni baada ya shule hizo kufunguliwa.

Aliwataka watendaji kata kwa kushirikiana na watendaji wa vijiji kuhakikisha wanafunzi wote wanahudhuria shule na pale penye changamoto wachukue hatua kali.

"Mtendaji wa kata ya shule husika kama mwanafunzi wa kata nyingine hajafika mpe taarifa ofisa tarafa husika ili afuatilie na kuhakikisha anahudhuria masomo," alisema.


Hata hivyo, aliwasisitiza wazazi hasa jamii ya kifugaji, kuendelea kupeleka watoto wao katika shule walizopangiwa na kuepuka kuchunga mifugo.

Katika shule zilizotembelewa ipo shule mpya ya Lengijape iliyopo katika Kijiji cha Namalulu Kata ya Naberera yenye mikondo miwili ikiwa na madarasa mawili ya awali, nyumba za walimu na matundu 24 ya vyoo, ambayo serikali imeijenga kwa Sh. milioni 638.

Alikagua Shule ya Sekondari Naisinyai ambayo imeongezewa miundombinu mipya ikiwamo madarasa tisa na madawati yake, mabweni matano na matundu 18 ya vyoo iliyogharimu Sh.milioni 924.

Pia mkuu huyo wa Wilaya alitembelea Shule ya Msingi Saniniu Laizer, ambayo hapo awali ilijengwa na mfanyabiashara maarufu wa madini Bilionea Saniniu Laizer na kuikabidhi serikalini, imeongezewa madarasa mawili ya wanafunzi wa awali.

Shule nyingine alizotembelea ni Shule ya Sekondari ya Simanjiro, Tanzanite na Mirerani B.W. Mkapa.





# Chadema Mara yalaani matukio watu kutekwa

**Na Timothy Itembe** MARA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Mara, kimelaani matukio utekaji yanayofanywa na watu wasiyojulikana na kuzitaka mamlaka husika kuchukua hatua kwani vitendo hivyo vinasababisha uvunjifu wa Amani.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Chadema Mkoa, Lucas Ngoto, kwenye mkutano wa Chama hicho ulioandaliwa kwaajili ya uchaguzi wa viongozi wa ndani wa chama ngazi ya Jimbo la Tarime mjini.

"Kumekuwapo na matukio ya hapa na pale ya watu kutekwa na kupelekwa kusikojulikana, matukio kama hayo sisi Chadema tunalaani na tunaomba serikali ichukue hatua ya kuyakomesha, "alisema Ngoto.

Mwenyekiti wa Jimbo la Tarime mjini, Selemani Abdala, alisema chama hicho kimejiimarisha hususani katika jimbo hilo la Tarime na wapo tayari kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa 2024. Alisema tayari amechukua fomu kwaajili ya kutetea nafasi yake na kama chama wanasubiri tu wakati ufike ili wasimike watu katika chaguzi hizo muhimu za ngazi za vitongoji, vijiji na mitaa kwaajili ya maandalizi ya uchaguzi mkuu wa 2025.

Akizungumza katika Mkutano huo mwanasheria wa kujitegemea, Bobu Chacha Wangwe alitangaza nia ya kugombea Ubunge Jimbo la Tarime mjini kupitia chama hicho.

Aidha alikisihi chama hicho kuhakikisha wanamtumia kikamilifu katika kukabiliana na kesi mbalimbali ili aitumie vyema taaluma yake katika utetezi wa chama na wananchi.

Ghati Nyerere alisema ipo haja kwa vyama vya kisiasa kuweka uwiano wa kijinsia katika kuwania nafasi mbalimbali kuanzia ngazi za chini hadi za juu ili kuwapa pia wanawake kushiriki kikamilifu katika siasa.

# Aweso akerwa utendaji kazi wa wakurugenzi KASHWASA

**Zatifa Ramadhani,** SAUT

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amekerwa na utendaji kazi wa wakurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA) kunakosababisha adha ya upatikanaji huduma hiyo wilayani humo.

Hali hiyo inaelezwa kusababisha watu zaidi ya milioni moja kuwa hatarini kukosa maji hivyo kuwaweka katika hatari ya kupata magonjwa kama vile kipindupindu.

Akizungumza baada ya kutembelea na kukagua Kituo cha Uzalishaji Maji cha Ihelele kilichopo wilayani Misungwi mkoani Mwanza, Waziri Aweso, aliwataka watendaji hao wajitathmini, waache visingizio na wafanye kazi kwa weledi.

Alisema serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 900 kuendesha mradi huo ikiwamo kununua dawa, umeme na kuwalipa mishahara watumishi hivyo ni lazima kazi inayofanyika iendane na thamani ya fedha.

Aidha, Waziri Aweso alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kufanya tathmini ya madeni ya Wizara ya Maji inayodai na inayodaiwa na aiwasilishe katika ofisi yake ndani ya wiki moja. Awali akisoma taarifa ya hali ya huduma katika Mamlaka hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa KSHWASA, Mhandisi Patrick Nzamba, alisema wamefanikiwa kuongeza idadi ya uzalishaji maji kutoka wastani wa mita za ujazo 18,000 kwa siku mwaka 2009/2010 hadi mita za ujazo 73,179 mwaka 2023/2024.

Aidha alisema kituo hicho kimekuwa na madeni makubwa ya muda mrefu kwa wateja wake, hadi kufikia Desemba 31,2023 ilikuwa inadai Sh.bilioni 14.096, kati ya hizo Sh.bilioni 12.662 wanaidai Mamlaka za Maji, Sh.bilioni 1.317 Jumuiya za Watumiaji Maji na Sh.bilioni 0.116 ni Migodi.

Alisema kutokana na upungufu wa dawa ya kutibu maji uliopo huenda wakazi zaidi ya milioni moja wakakosa huduma ya maji kutoka katika mradi huo unaotegemewa na mikoa mbalimbali ikiwemo Shinyanga, Geita, Singida na Tabora.

Aidha Waziri Aweso alihitimisha ziara yake katika Mradi wa Maji wa Butimba uliopo jijini Mwanza na kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo unaotarajiwa kukamilika hivi karibuni.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme akizungunza jana na waandishi wa habari mkoani Shinyanga, kutoa taarifa ya hali ya ugonjwa wa kipindupindu mkoani humo, kwamba kati ya wagonjwa 41 ambao walikuwa wakikabiliwa na ugonjwa wa kuhara na kutapika kuwa wagonjwa 18 wamebainika kuwa na kipindupindu na wamepatiwa matibabu, na kusalia wagonjwa watano wakiendelea kupata tiba kwenye kambi zilizotengwa, **PICHA: MARCO MADUHU**

# Familia mjamzito aliyefariki kwa kukosa huduma yaiangukia serikali

**Na Waandishi Wetu**

FAMILIA ya Marehemu Rechal William(19) aliyefariki dunia na kichanga tumboni baada ya kukosa huduma ya kujifungua katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama imetoa wiki mbili kwa serikali kuwawajibisha wale wote waliohusika na tukio hilo.

Akizungumza kwa niaba ya wanafamilia hao juzi Msemaji wa familia hiyo, Lazaro Mwandu, aliiomba serikali kuwawajibisha watumishi wote waliohusika katika tukio hilo wakiwamo madaktari kwa kuwanyang'anya leseni zao kwani wameitia doa serikali.

Alisema endapo muda huo utaisha bila kuona hatua zozote dhidi yao itawabidi kwenda ngazi za juu kwa ajili ya kulalamikia suala hilo ili lisijirudie katika hospitali hiyo na zote za serikali zinazoendekeza uzembe.

Aidha, Mwanambalu alitoa pongezi kwa serikali kwa kusikia vilio vya Watanzania kwa kujenga majengo mengi ya kuwahudumia jamii vikiwamo vituo vya afya na zahanati huku akiwasihii viongozi wa sekta husika kusimamia maadili ipasavyo kuondoa uzembe wa watumishi.

"Haiwezekani daktari anaambiwa awasikilize ndugu wa mgonjwa halafu anasema kuwa hana muda kama huo wakati wanalipwa mishahara ambayo inatokana na kodi tunazolipa sisi huku akiendelea kuchati na simu ya kiganjani," alisema.

Mama wa Marehemu, Agnes Pastory, alisema Agness alipelekwa katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama Desemba 28, mwaka jana akiwa na uchungu wa kujifungua majira ya saa nne na nusu usiku na kuambiwa na daktari wa zamu kuwa mapigo ya moyo ya mtoto hayapo.

Alisema kuwa majira ya saa sita usiku aliendа katika wodi ya kujifungulia na kumweleza dakatari juu ya tatizo alilonalo mtoto wake lakini majibu yalikuwa kuwa hana muda wa kumhudumia hadi alifariki dunia majira ya saa saba siku inayofuata kwa kutoka na damu nyingi.

Kufuatia tukio hilo wabunge wanawake mkoani Shinyanga, walilaani vikali na kuitaka familia hiyo kuwa wavumilivu kwani serikali imeanza kuchukua hatua ikiwamo kuunda tume mbili za uchunguzi dhidi ya kifo hicho na kuwasimamisha kazi watumishi wote waliokuwa zamu ili kupisha uchunguzi huo.

Mbunge wa Viti Maalumu, Dk. Christina Mnzava, akizungumza kwa niaba ya wabunge wenzake wa mkoa alisema kupitia timu hizo mbili zinazochunguza huduma ya matibabu pamoja na uongozi zitabaini ukweli juu ya tukio hilo na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wote waliohusika.

Alisema, wao kama wabunge wanawake hawawezi kufumbia macho vifo vitokanavyo na uzazi, wakati ambapo serikali inafanya jitihada kubwa kuimarisha miundombinu ya majengo ya kutolewa huduma hiyo.

Imeandikwa na Mohab Dominick na Shaban Njia, (KAHAMA).

Ukurasa 13



**MIAKA 60 MAPINDUZI**
**Yanavyogeuza visiwa viota vya utajiri, SMZ yavikodisha, vyajengwa hoteli tishio**

Ukurasa 1 4



**MOHAMED HEMEDTI DAGALO**
**Anapoelekea kuitwaa Sudan, baada ya Ghuba kumkubali, A/Mashariki nayo yampa tano**



MZOZO WABUNGE 19

# ACT-Wazalendo inavyowatamani viti maalum wanaozozaniwa CHADEMA

• Yawakaribisha, yawaita ni jeshi kubwa majimboni lisiachwe kupotea

**Na Sabato Kasika**

UKIWA umebakia mwaka mmoja kuingia kwenye uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani, Chama cha ACT- Wazalendo, kimewanyooshea mikono wabunge 19 wa CHADEMA wanaozozaniwa, kikisema milango iko wazi kupokea wanawake hao mashujaa kwenye siasa.

ACT-Wazalendo, inawasihi kuwa iwapo wataamua kuachana na 'mama' CHADEMA na kutafuta nyumba ya kuendesha harakati za kisiasa wajiunge na chama hicho.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, anawaalika, akitoa sababu kadhaa za kuwataka wanasiasa hao, anaposema Halima na wenzake ni kielelezo cha mapambano ya wanawake kwenye siasa.

Hata hivyo, wabunge hao licha ya kuwa wameshapata taarifa za mwaliko hawakuwa tayari kukubali, kukataa wala kuzungumzia makaribisho hayo.

Nipashe inapowasiliana na baadhi yao kupata maoni ya ofa ACT, kama wapo tayari kujiunga ili waendelee na harakati za kisiasa hawakuwa tayari kuzungumza.

Mmoja wa wabunge hao ambao wamepewa jina la utani la COVID-19, Esther Bulaya, anapoulizwa, anajibu hawezi kuzungumzia jambo hilo na kukata simu.

Mbunge mwingine Sophia Mwakagenda, licha ya kupokea simu, anaomba apigiwe baada ya dakika, hata hiyo, muda ulipotimu, hakupokea simu.

Esther Matiko, anapotafutwa, baada ya kupokea simu na kupewa maelezo anajitetea kuwa hataweza kuzungumzia makaribisho kwa sababu yuko katika ofisi ya mtu na kuomba atumiwe ujumbe au meseji. Hata hivyo, hakujibu meseji ya Nipashe wala kupokea simu, anapotafutwa tena.



Baadhi ya wabunge 19 ambao wanaombwa kujiunga na ACT-Wazalendo. **PICHA: MTANDAO**



Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu.

Katibu wa CHADEMA, John Mnyika, anapoelezwa iwapo anakubali au ana maoni mengine, kuhusu ACT-Wazalendo kuwapa nafasi wanachama wake, anasema walishamwandikia barua Spika Dk. Tulia Ackson, ya kuomba waondolewe.

Anaongeza kuwa wamemtaarifu kuwa wabunge hao hawana kinga yoyote ya kimahakama na wanatakiwa waondolewe bungeni.

"Mtafuteni Spika wa Bunge atoe kauli kutokana na barua niliompelekea," anasema Mnyika.

Kwa upande mwingine Ado, Shaibu anasema wanakaribishwa na chama hicho wakati wowote na kuongeza: "Ninatamka kwa kujiamini kabisa kwamba Halima Mdee na wenzake tunawakaribisha kwa mikono miwili ndani ya ACT- Wazalendo. Nafasi ipo kuendeleza mapambano ya kuwatetea na kuwapigania Watanzania."

Anataja sababu za kuwataka wabunge hao kuwa ni ukweli kuwa makosa anayoyasikia dhidi yao, yanasameheka.

"Sababu nyingine ni kwamba, wengi wao walifanya vizuri kwenye uchaguzi majimboni 2020 na hatuwezi kuliangamiza jeshi kubwa lote hili. Tunawakaribisha kwa mikono miwili," anasema.

Anaongeza kuwa nafasi ipo ya kuendeleza mapambano ya kuwatetea na kuwapigania Watanzania kupitia chama hicho, na pia ni hasara kwa taifa na kwa harakati za ukombozi wa wanawake na demokrasia kuwapoteza wabunge hao mashupavu.

"Kimsingi, kila mwanasiasa na hata binadamu hukosea, ni muhimu kupima makosa na thamani ya mtu. Hilo ni la msingi zaidi, hivyo, ninatamka kuwa wakati wowote Mdee na wenzake wakihitaji kujiunga na chama hiki, milango ipo wazi," anasema.

**KINACHOENDELEA**

Desemba 14, mwaka jana, Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, ilitengua uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kuwafukuza uanachama Halima Mdee na wenzake 18 wakati wa kusikiliza rufani za wabunge hao.

Uamuzi huo wa Jaji Cyprian Mkeha, unatokana na kubainika kuwa wajumbe 23 waliotoa hukumu hiyo kupitia Kamati Kuu ya chama hicho, kuhusika kusikiliza rufani zao na kuitolea uamuzi katika Baraza Kuu.

Kuhusu hoja ya waleta maombi kudai hawakupewa muda wa siku 14 kujitetea, mahakama ilibainisha kuwa walipewa nafasi ya kusikilizwa na hawakuitumia.

Anaeleza kuwa Kamati Kuu kwa mujibu wa Katiba ya CHADEMA, ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri lao kwa njia ya dharura, na kwamba taratibu zote ambazo walistahili kuzizingatia zilizingatiwa.

Hata hivyo, akafafanua kuwa uamuzi wa Baraza Kuu wa kusikiliza rufani za wabunge hao uliofanywa na baadhi ya wajumbe walioshiriki kutoa uamuzi ndani ya Kamati Kuu, akisema hatua hiyo si sahihi.

Katika ufafanuzi wa hukumu hiyo, Wakili Dickson Matata, anasema, uamuzi wa kuwafuta uanachama ni halali, na kwamba mahakama ilitengua uamuzi wa rufani ya Baraza Kuu.

**INAENDELEA UK. 14**

# Vijana wanavyoona ukakasi miswada sheria za uchaguzi




Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi. **PICHA:MTANDAO**

**Na Halfani Chusi**

WAKATI wadau wakitoa maoni kuhusu miswada iliyowasilishwa bungeni kurekebisha sheria zinazohusika na uchaguzi, vijana ambao wanaamini kuwa ndiyo wapigakura wengi zaidi, wanaikataa, wakisema haina maslahi kwao.

Viongozi wa vijana kutoka Ngome ya Vijana - ACT Wazalendo, CUF (JUVICUF) na NCCR Mageuzi wanapinga miswada mitatu inayohusu sheria ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani, sheria ya tume ya uchaguzi na ile ya vyama vya siasa iliyowasilishwa na kusomwa bungeni kwa mara ya kwanza Novemba mwaka jana

Wanasema miswada hiyo haijabeba hoja zenye ustawi wa vijana, Katibu wa Vijana CUF Taifa, Iddi Mkanza, akizungumza kwa niaba ya viongozi wengine anaeleza.

Anafafanua kuwa wamebaini kuwa vifungu vingi vya miswada hiyo vimekinzana na katiba ya mwaka 1977, hali hiyo haitaleta usawa na haki, haitaimarisha demokrasia wala kupanua ushiriki wa kisiasa kwa wananchi hasa vijana ambao ndiyo idadi kubwa ya Watanzania.

Anaongeza kuwa kinachobadilishwa hakitaleta uwajibikaji kwa viongozi sababu ya kutokuwa na uchaguzi huru na haki na hivyo kuendelea kuwa na mazingira hatarishi ya amani kipindi cha uchaguzi.

**WANACHOTAKA**

Mkanza anasema, baada ya kupitia mapungufu hayo wanapendekeza kuondolewa kwa kifungu cha 6(1) na 6(2) katika muswada wa sheria ya uchaguzi kinachohusu kuwatumia wakurugenzi wa halmashauri na watumishi wa umma kusimamia uchaguzi.

Anaendelea kukitaja kifungu cha 18(2)kuwa kinahitaji kurekebishwa, muundo wa Tume ya Uchaguzi ugawike sehemu mbili; bodi na menejimenti na kwamba bodi iwe chini ya Mwenyekiti wa NEC na iajiri mkurugenzi wa uchaguzi kwa sifa zitakazoainishwa na kwa uwazi.

Anapendekeza kifungu cha 9(3) kifutwe kumwondoa mkurugenzi wa uchaguzi kuwa katibu wa kamati ya usaili na badala yake katibu wa kamati ya usaili awe Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG).

> “Dunia imebadilika nchi nyingi zinaruhusu wafungwa kupiga kura bila kikwazo. Mfano Kenya, Denmark, Finland, Ufaransa, Zimbabwe, Japan, Poland na Peru...” anasema Katibu Mkanza.

Sifa za wajumbe wa tume katika kifungu cha 7(2) cha muswada wa sheria mpya ya tume hiyo uzingatie vijana. Kifungu kitamke angalau wajumbe wawili kati ya watano wawe vijana.

Vifungu vya 35(1)(2) na 51(1) katika muswada wa sheria ya uchaguzi vifutwe sababu vipo kinyume na katiba ya mwaka 1977 ibara ya 21(1)(2) inayoruhusu uhuru wa mtu kushiriki katika masuala ya kiuongozi na uamuzi.

“Pia kinazuia ushiriki wa vijana, kwamba hakuna haja ya mgombea kuweka dhamana kwa msimamizi wa uchaguzi ni jambo ambalo halina mantiki, ikiwa mgombea amepitishwa na chama chake inatosha kumwamini badala ya kuweka vikwazo vya dhamana ya fedha.

“Mgombea apewe haki kwa mujibu wa katiba ibara ya 13(6)(a) kama hajaridhika na uamuzi wa Tume ya Uchaguzi kukata rufani na kupinga uamuzi huo Mahakama Kuu. Kitendo cha kuzuia kukata rufani ni kinyume cha ibara ya 107(A) ya katiba inayotoa mamlaka kwa mahakama kama chombo cha uamuzi wa mwisho katika utoaji haki ndani ya serikali.

“Kuzuia watu kukata rufani kupitia mahakama ambayo ndiyo njia ya amani na usawa katika kutafuta haki tafsiri yake ni kuwatengenezea mazingira ya kusaka haki yao kwa njia nyingine jambo ambalo sio muafaka kwa ustawi na mustakabali wa taifa,” anaongeza Mkanza.

Kufanyika marekebisho katika muswada wa sheria ya uchaguzi kifungu cha 85(1) na 14(1) ili kiruhusu wananchi kupiga kura ya udiwani, ubunge na urais popote walipo hata kama ni tofauti na maeneo waliyojiandikishia kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni pendekezo jingine.

Mkanza anaendelea na mapendekezo yake kwamba, muswada wa sheria ya uchaguzi ujumuishe pia chaguzi za serikali ya mtaa na uitwe muswada wa sheria ya uchaguzi wa rais, wabunge, madiwani na viongozi wa serikali ya mitaa, vijiji na vitongoji.

Kifungu cha 10(1)C cha muswada wa sheria ya uchaguzi kinachozuia wafungwa kupiga kura kifutwe kwasababu kinakinzana na ibara ya 5(1) ya katiba ya mwaka 1977, pia hukumu ya mahakama kuu katika kesi No.3 ya 2022 ya Tito Magoti, anasema.

“Dunia imebadilika nchi nyingi zinaruhusu wafungwa kupiga kura bila kikwazo. Mfano Kenya, Denmark, Finland, Ufaransa, Zimbabwe, Japan, Poland na Peru...” anasema Katibu Mkanza.

Fedha za kuendesha shughuli za tume zitoke kwenye mfuko mkuu wa serikali ili kuongeza uhuru na ufanisi wa tume katika kutekeleza majukumu yake tofauti na sasa hivi tume ya uchaguzi inatengewa na kupewa fedha kama hisani kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Kuondoa mamlaka za serikali (Msajili wa Vyama vya Siasa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali) katika kuweka mapingamizi dhidi ya wagombea. Kifungu kiruhusu yeyote kuweka pingamizi na si Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kuondolewa gharama za kupata kadi kitambulisho kipya cha mpigakura vijana tunapendekeza maneno “ada” yafutwe na kuondolewa ili kuongeza hamasa ya wananchi na vijana kupiga kura na pia ili kiende sambamba na matakwa ya katiba ya mwaka 1977 ibara ya 5(1) na 21.

“Serikali, kamati za bunge na wabunge kuhusika na kuheshimu sauti na maoni ya wananchi, vijana, vyama vya siasa, asasi za kiraia, wanaharakati, viongozi wa dini na wadau wote kuhusu upungufu na kasoro katika miswada hii ili upungufu na kasoro zote viondolewe kukidhi matarajio ya wananchi kwa mustakabali wa Demokrasia, amani, uwajibikaji na maendeleo ya nchi yetu,” anasema.

Mwanasiasa huyo anasema serikali ipeleke muswada wa marekebisho madogo ya katiba ya mwaka 1977 katika vipengele ambavyo vinahusu chaguzi sambamba na miswada hiyo.

Aidha, wanataka serikali iweke wazi ratiba ya mchakato wa mabadiliko ya katiba ili Watanzania wajue nini kinaendelea.

MIAKA 60 MAPINDUZI

# Yanavyogeuza visiwa viota vya utajiri, SMZ yavikodisha, vyajengwa hoteli tishio

## • Chumba kutozwa mil. 13/- kwa siku



Ujenzi wa hoteli ya nyota tano ukiendelea katika kisiwa cha Bawe, ambacho ni miongoni mwa 16 vilivyokodishwa na wawekezaji. **PICHA: MWANDISHI WETU**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

UNGUJA na Pemba kuna baraka ya visiwa vidogo 52 ambavyo kabla ya Mapinduzi ya 1964, havikuwa na tija mbali ya kuwa makambi ya wavuvi au madago.

Kwa muda wote huo visiwa hivyo vilikua havina jukumu kiuchumi zaidi ya kutumiwa na wavuvi wanaokaa dagoni au kambini kwa ajili ya kuvua, kuanika na kuuza samaki.

Baada ya uongozi wa awamu ya nane kuingia madarakani na sera ya uchumi wa bluu, uamuzi wa kuvikodisha visiwa hivyo ili kukuza uwekezaji na kupata mapato umetimia.

Wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, uongozi wa awamu ya nane umevikodisha visiwa hivyo, vilivyokaa miongo mingi bila ya kuendelezwa wala kuchangia ukuaji wa nchi.

Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imekodisha visiwa 16 Unguja na Pemba ambapo hayo ni mafanikio katika kukuza uchumi wa nchi, Mkurugenzi wa ZIPA, Sharif Ali Sahari, anasema.

Anaongeza kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya Dk. Hussein Ali Mwinyi, miradi ya uwekezaji 269 yenye mtaji wa dola bilioni 4.5 ambayo inatarajiwa kuleta ajira 17,000 inatekelezwa, akisema ni mafanikio makubwa ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi.

Sharif anasema miradi hiyo kwa asilimia 70 inahusiana na uwekezaji wa hoteli za kitalii ambazo baadhi zimejengwa katika visiwa 16 vilivyokodishwa na jumla ya miradi yote iliyowekezwa katika sekta hiyo ya utalii ni 112.

Akizungumzia uwekezaji katika visiwa vidogo ambavyo kwa miaka yote vilikuwa havitumiki na vingine kugeuzwa vichaka vya uhalifu, anasema vinatarajiwa kuingiza dola 300,000,000 (takribani Shilingi bilioni 75.3).

"Ni mafanikio ya uwekezaji katika miaka hii 60 ya Mapinduzi ...serikali imefanya makubwa katika sheria ya ZIPA na sasa kuifanya Zanzibar kituo bora katika Afrika ya Mashariki na Kati kiuwekezaji," anasema.

Aidha, anaongeza kuwa miradi iliyowekezwa katika sekta ya utalii ni 112, ikihusisha majengo 56 na katika viwanda ni miradi 36 na yote hayo yamefanikiwa baada ya serikali kuondoa ukiritimba kwa wawekezaji na kuunda kituo cha 'one stop center' ili wawekezaji kutopata usumbufu.

Sharif anasema mwekezaji anapata kibali cha ukaazi ndani ya saa 24 wakati cheti ya uwekezaji hakichelewi ni ndani ya saa 24 iwapo atawasilisha nyaraka zote muhimu.

Kadhalika, katika kipindi cha miaka mitatu vibali vya ukaazi 2,089 vimetolewa wakati vya ajira vilivyotolewa ni 2,587 kupitia huduma kwa wawekezaji.

Anasema miongoni mwa visiwa 16 vilivyokodishwa ni Bawe ambapo mwekezaji amewekeza dola milioni 38 (zaidi ya Shilingi bilioni 9.5) na uwekezaji huo utakuwa na majengo 159 zikiwamo hoteli za kifahari zenye hadhi ya nyota tano na mradi huo unatarajiwa kufunguliwa Machi mwaka huu.

Kingine ni Pamunda, kitakacho kuwa na hoteli ya kifahari ya kuhudumia matajiri wakubwa duniani wanaotarajiwa kufikia huko ambapo kwa siku moja watakuwa wanalipia Shilingi milioni 13.

Sharif anasema katika Hoteli ya Tulia Pamunda Island inayojengwa kisiwani humo pia kutakuwa na mchezo mkubwa wa kitajiri duniani unaoitwa 'Formular One' au mbio za magari hivyo matajiri wakubwa watafika katika kisiwa hicho.

Anayataja mafanikio mengine yaliyofanyika kukamilika kwa mfumo wa uidhinishaji wa miradi kwa njia ya kidijitali "Online" ambapo kwa sasa mwekezaji anaweza kusajili mradi wake kwa njia hiyo.

Mkurugenzi huyo anasema hatua hiyo kwa kiasi kikubwa imepunguza urasimu na kurahisisha kila jambo hatua ambayo ndiyo moja ya sababu ya wawekezaji kuvutiwa kuwekeza Zanzibar.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhamed Said, anasema maboresho makubwa yanayofanywa na serikali katika sekta ya uwekezaji yamefunguwa milango zaidi kwa wawekezaji kuja Zanzibar.

Serikali imeamua kufuata sera ya uchumi wa buluu kama ni mpango mkuu wa maendeleo ya Zanzibar ambao unahusisha matumizi ya rasilimali za baharini na maeneo yaliyozunguka katika shughuli za kiuchumi.

Aidha, anasema ni vyema ikafahamika kuwa kutokana na mpango huo, imeamua kuvikodisha visiwa hivyo vidogo kwa ajili ya uwekezaji baada ya kukaa muda mrefu bila ya kuendelezwa na kushindwa kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi na jamii ya visiwani.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, anasema visiwa 16 vilivyokodishwa ni urithi hivyo wawekezaji wanasharti la kutunza mazingira kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Aidha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Jamal Kassim Ali, kazi kubwa iliyofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuimarisha deplomsia ya uchumi imeifungua nchi kwa kutangaza fursa za uwekezaji wa nje na kuwa na imani ya kuleta miradi yao mikubwa nchini.

Kadhalika, anasema kuimarika kwa miundombinu ya kiuchumi na huduma za kijamii kutasaidia kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji na kuinua maisha mazuri ya wananchi wa Zanzibar na katika kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unaimarika serikali imeamua kufuata sera ya uchumi wa buluu kama mpango mkuu wa maendeleo ya nchi ambao unahusisha rasilimali za baharini.

"Kutokana na mpango huo serikali imeamua kukodisha visiwa vidogo kwa wawekezaji ili kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi, inatambua umuhimu wa kutunza rasilimali zetu pamoja na maslahi ya wananchi katika miradi inayotekelezwa kwenye visiwa vidogo na maeneo mengine," anasema Waziri Ali.

Filamu ya Royal Tour imefanikisha kuvutia wawekezaji wengi hivyo baada ya miaka miwili kunahitajika kuwepo kwa filamu nyingine ya awamu ya pili, ili kuvutia watalii zaidi, anashauri.

Ulinzi wa mazingira kwa wawekezaji wanaowekeza miradi ya kitalii ili kuepuka uharibifu wa fukwe za bahari ni suala la msingi, anasema Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Selemani Jafo.

Jafo anasema miradi ya hoteli kwa kiasi kikubwa inahitaji kuwapo kwa mikakati ya kulinda mazingira zikiwamo fukwe na kuhakikisha hakuna uharibifu utakaotisha maisha ya binadamu na viumbe baharini.

Anasema dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi ambayo ni matokeo ya kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe na makazi ya watu maeneo ya mwambao akihimiza ulinzi wa mazingira unahitajika.

MOHAMED HEMEDTI DAGALO

# Anapoelekea kuitwaa Sudan, baada ya Ghuba kumkubali, A/Mashariki nayo yampa tano



Kiongozi wa Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan.



Mkuu wa kundi la Rapid Support Forces nchini Sudan, Mohamed Hamdan Dagalo. **PICHA: REUTERS**

**Na Ani Jozeni**

KIONGOZI wa kundi la RSF (Rapid Support Forces) nchini Sudan, Mohamed Hamdan Dagalo au Hemedti, amezuru Afrika Mashariki, Pembe ya Afrika na kuzungumza na viongozi wake, hatua inayoonyesha kuwa huenda anakubalika.

Hivi karibuni anakaribishwa Ethiopia, Uganda na Kenya akifanya mazungumzo na Rais Yoweri Museveni wa Uganda na ndani ya wiki moja akakutana na Rais William Ruto, ila akiwa Ethiopia alikutana na serikali na hata na viongozi wa makundi tofauti ya wanaohusika na mzozo wa kisiasa Sudan.

Katikati ya mkwamo wa majadiliano na serikali ya Khartoum, pengine Afrika inaanza kujiandaa kwa utawala mwingine Sudan na ikiwezekana isaidie kupata ufumbuzi wa tatizo hilo kwa haraka.

Hisia kuwa Hemedti sasa anakubalika kwa nchi za Afrika zinazoizunguka Sudan ni 'tonge' ambalo wengi kati ya wanaoitazama Sudan wanapata taabu kulimeza.

Kiongozi huyu wa RSF, amewahi pia kuongoza kikosi cha Janjaweed, kwa tafsri ya Kiarabu 'jin' au 'pepo' anayesafiri kwa farasi (jawad ni farasi) wakitumia wanyama hao walifanya mauaji na uhalifu wa kivita katika jimbo la Darfur miaka kadhaa iliyopita. Janjaweed wanaaminiwa kuwa waliundwa kwa lengo la kusafisha makabila yasiyokubalika nchini Sudan.

Kielelezo cha ufaulu wa Dagalo na kukubaliwa kwake na nchi za jirani ni kwamba hata Falme za Ghuba zinawekeza kwake na RSF kama kundi wanaloweza kulitegemea kupitisha agenda na mwelekeo wanaotaka.

Wanaamini kuwa wako karibu na wakuu wa koo za kimwinyi, wafuasi wa Rais Omar Hassan al-Bashir aliyepunduliwa katika wimbi la madai ya demokrasia mwaka 2019 na sasa yuko kizimbani.

Mtawala wa Sudan aliyeko madarakani, Jenerali Abdel Fattah al-Burhani, alianza kukubali utawala wa kiraia urejeshwe na vikosi vya RSF viunganishwe na jeshi, wakati ni mradi mkubwa wa kukusanya madini, kuzuia nchi hiyo isielekee kwenye mitizamo ya nchi za magharibi.

Ndiyo maana Falme za Ghuba zinamkubali Hemedti, na wanaoumuunga mkono Al-Burhani hawataki kujiingiza huko, kwa mfano Misri ya Jenerali Abdel Fatah al-Sisi, inaona kuingia kwa Hemedti siyo tatizo kwao.

Ila kuungwa mkono na Falme za Ghuba, kuiteka Darfur na hata mji muhimu wa Wad Medani kando ya jiji la Khartoum inaweza isiwe turufu kwa Hemedti, kwani wananchi wa Sudan wameanza kuamka katika usingizi wa maelezo ya vyombo vya habari na Sudan ni vya majenerali wawili wanaohitilafiana.

Kama ilivyokuwa Ukraine na hata Israel baada ya uvamizi wa Hamas, wanaondoka katika makambi ya ukimbizi na kutafuta vituo vya jeshi kuandikishwa, wapewe mafunzo ya vita na kusaidia kuikomboa Sudan kutoka katika mikono na kundi la Janjaweed na washirika wao katika Falme za Ghuba, kuweka utawala mwingine.

Ni kulinda wimbi la mapinduzi dhidi ya mamluki ambao kwanza walitumiwa na al-Bashir na sasa wanataka watawale wenyewe.

Ziara ya kiongozi huyo wa kundi la mamluki inaweza kuonekana inadhihirisha kuwa uwezekano wa ushindi wa kundi hilo unaongezeka, ila ukiangalia kwa karibu nini kinatokea unapata mashaka ya jawabu hilo la haraka.

Kuna uwezekano kuwa Dagalo au Daglo akiangalia mwenendo wa vita kwa sasa, anaweza kupata picha ya uwezo mkubwa zaidi aliofikia kwa sasa na ataka shinikizo liongezwe kwa serikali ya Khartoum kukubali yaishe, irudi katika meza ya mazungumzo kwa nia ya kugawana madaraka kwani RSF imeteka takriban nusu ya nchi.

Si rahisi kusema nini anachoona Dagalo mbele ya safari, ila atakuwa amesikia kuwa wakimbizi na wasomi kwa makundi sasa wanatafuta njia za kujiunga na jeshi rasmi, baada ya kuielewa dhamira ya mamluki.

Kwa upande mwingine, uandikishaji wa mamluki hao zaidi ni kutoka familia za Kiarabu na zaidi wenye fedha au ardhi, waliokuwa na maslahi zaidi na utawala wa al-Bashir, na wasiotaka kusikia lolote kuhusu demokrasia na utawala wa kiraia.

Ni mamluki kwa vile hawaipendi nchi tofauti na maslahi ya kundi maalum, na kuvutwa kwa pesa za nchi za Ghuba kupata nyenzo, posho na misaada.

Tofauti, kuingia jeshi rasmi hasa ni hamasa ya uzalendo, kuwa kundi hilo linataka kuiteketeza nchi, iwe jela ya wahodhi ardhi wakitunga sharia za kuwezesha wanaobaguliwa kufahamika kama 'dhimmi,' yaani wasio Waislamu halisi na wanatozwa kodi kwa nguvu.

Halafu wako mamluki wa kawaida ambao si wa tabaka linalohodhi lakini wanapenda kuwa na kipato hata kama ni pamoja na kushika silaha, na hata ingekuwapo hatari ya kutumwa vitani na kupoteza maisha.

Kundi hili lingeweza kubadili sura ya Sudan pale fedha za Ghuba zinaponunua watu takriban wote wenye tamaa hiyo, na nchi ikabidhiwe kwa Dagalo, na Sudan igawanywe kwa familia za tabaka lenye utajiri na uhusiano na Al Bashir.

Ila pale wasomi wa ngazi tofauti na raia wa maeneo yanayobaguliwa wakianza kujazana jeshini, na endapo kuna njia za utawala wa Al-Burhani kuwahudumia kama askari, nguvu hiyo inaweza kuizidi ile ya mamluki, hivyo wimbi la ushindi ambalo limemwezesha Dagalo kujipeleka Ethiopia, Kenya na Uganda kama mtu aliyeteka nusu ya nchi hiyo na anaweza kukamilisha mipango ya kuteka nchi yote, litaanza kufifia.

## ACT-WAZALENDO INAVYOWATAMANI VITI MAALUM WANAOZOZANIWA CHADEMA

**INATOKA UK. 11**

Sababu ya kufanya hivyo ni wajumbe ambao ni mwenyekiti na katibu wa kamati kuu iliyohusika kuwafuta uanachama kuwamo tena katika kikao cha wajumbe wa Baraza Kuu kubariki maamuzi ya Kamati Kuu.

**MWANZO WA MVUTANO**

Novemba 24, 2020 baada ya uchaguzi mkuu, wabunge hao wa viti maalum waliapishwa jijini Dodoma na Job Ndugai, wakati huo Spika wa Bunge na kuzusha sintofahamu baada ya CHADEMA kudai haikuwateua.

Wabunge hao ni Halima Mdee, Esther Matiko, Grace Tendega, Cecilia Pareso, Ester Bulaya, Agnes Lambart, Nusrat Hanje, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Asia Mohammed na Felister Njau.

Wengine ni Naghenjwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda, Kunti Majala, Stella Flao, Anatropia Theonest, Salome Makamba na Conchesta Rwamlaza.

Baada ya kuwaapisha, Spika Ndugai alikemea wanaodharau shughuli zinazofanywa na bunge hilo, akisema mambo yasiyokubalika, hasa kudharau ni kudhalilisha uongozi wa bungeni wabunge walioapishwa.

Katika ufafanuzi wake Ndugai, akasema, maboresho ya kanuni inayosimamia kiapo yanamwezesha mbunge mpya kutekeleza kazi za kibunge na kuwajibika kwa wananchi baada ya kuchaguliwa kwake au kuteuliwa.

CHADEMA iligoma kuteua wabunge wa viti maalumu wakidai kuwa hawatambui matokeo ya uchaguzi, iliyodai ulikuwa na kasoro nyingi na kusababisha wapate mbunge mmoja Aida Kenan wa Jimbo la Nkasi Kaskazini mkoani Rukwa.

Viongozi wa chama hicho wakiongozwa na Mwenyekiti Freeman Mbowe, walidai kutoteua wabunge wa vitu maalum kwa kuwa kuwateua ingekuwa ni sawa na kuhalalisha uchaguzi huo.

Kutokana na mazingira hayo ya wabunge hao 19 kwenda kuapisha bila kile ambacho kinaelezwa kuwa ni uongozi wa chama kutojua, Kamati Kuu ya CHADEMA ikawavua uanachama.

Tangu wakati huo, wabunge walipokimbilia mahakamani kupata haki, kesi yao imeendelea kunguruma hadi Desemba mwaka jana Jaji alipobatilisha kilichofanywa na kamati kuu.



## Wawekezaji diaspora walia TBS kuchelewesha vibali

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BAADHI ya wawekezaji wa Kitanzania wanaoishi nje ya nchi waliohamasishwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuja kuwekeza wamedai kucheleweshewa vibali vya ubora wa bidhaa toka Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Akizungumza na waandishi wa habari mmoja wa wawekezaji, Pheno Kashimbiri, aliomba TBS kuharakisha utoaji wa vibali ili kuwapa nguvu ya kuendelea kuwekeza hapa nchini.

"Rais Samia amekuwa akiwahamasisha Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuja kuwekeza nyumbani, lakini changamoto inayokwamisha na ucheleweshaji wa kuvipata vyeti vya ubora vinavyotakiwa kutolewa na TBS," alisema.

Kashimbiri alisema kuwa ikiwa TBS, itarahisisha mchakato huo wawekezaji walio wengi wataweza kuipunguzia mzigo wa kuajiri vijana kutokana na uwekezaji unaofanyika hapa nchini. "Baadhi yetu tayari tumeitikia wito huo wa Rais wetu mama Samia wa kuja nyumbani kuwekeza lakini bado michakato ya kupata vibari una changamoto," alisema.

Alisema hali hiyo inatia hofu baadhi ya wawekezaji na kusita kuja kuwekeza kutokana na utendaji wa Shirika la Viwango kuwa mgumu.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa kazi na huduma mbalimbali ya kampuni hiyo ya Norland, Msimamizi wa kituo cha Dodoma, Bashiri Iddi, alisema kuwa uwepo wa uwekezaji huo hapa nchini utasaidia kutoa ajira kwa makundi mbalimbali.

Alisema kuwa Watanzania walio wengi watajipatia kipato kwa njia ya halali na watakuza maisha kutokana na kampuni hiyo kuwa na bidhaa zinazosambazwa kwa wateja.

# Wataka tarehe kupiga kura ibainishwe kwenye sheria

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa demokrasia nchini wameshauri Sheria ya Uchaguzi kubainisha tarehe rasmi ya uchaguzi tofauti na sasa ambapo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ndiyo yenye jukumu la kupanga siku hiyo.

Walibainisha hayo jana jijini hapa, walipokuwa wakitoa maoni kuhusu miswada minne ya uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba, Ananilea Nkya, alisema wanapendekeza sheria ya uchaguzi itamke bayana siku rasmi ya wananchi kupiga kura kwa ajili ya kuchagua viongozi wa nafasi ya urais, ubunge na madiwani.

"Sheria imekaa kimya kwenye kubainisha siku rasmi ambayo itatumika kwa ajili ya wananchi kupiga kura kuchagua viongozi wao kwenye uchaguzi.

"Hii inafanya Tume ya Taifa kuwa na jukumu la kupanga siku ya uchaguzi ambayo wakati mwingine imekuwa ikiibua hoja mbalimbali na wengine kukataa uchaguzi kufanyika siku ya Jumapili," alisema.

Alisema ili kuondoa sintofahamu hiyo sheria ya uchaguzi itatakiwa kubainisha siku rasmi ambayo itatumika kupiga kura kwa ajili ya kuchagua viongozi.

"Kama inawezekana sheria ibainishe kuwa uchaguzi utafanyika kila Jumatano ya mwisho ya mwezi Oktoba ili ifahamike rasmi na kuiondolea Tume ya Taifa ya Uchaguzi kupanga tarehe kila inapofika mwaka wa uchaguzi," alisema.

Aidha, alisema sheria ya uchaguzi inapaswa pia kutamka bayana wajibu wa vyombo vya habari katika uchaguzi wa Rais, wabunge pamoja na madiwani.

"Lazima sheria ya uchaguzi ieleze wazi majukumu ya vyombo vya habari vya serikali, vyombo vya vyama na vya watu binafsi nini majukumu yao katika kuhakikisha wanawapa fursa sawa wagombea wa vyama vyote kwenye kunadai sera zao," alisema.

Mkurugenzi wa Mikakati na Kujifunza wa Shirika la TWAWEZA, Baruani Mshale, alisema sheria hiyo inapaswa kufanyiwa marekebisho katika mambo mbalimbali ikiwamo kuruhusu matumizi ya teknolojia kutunza nyaraka za uchaguzi.

Alisema hivi sasa sheria inasema nyaraka za uchaguzi zinahifadhiwa kwa kipindi cha miezi sita na baada ya hapo zinateketezwa lakini kama itatumika teknolojia itasaidia nyaraka hizo kutunzwa kwa muda mrefu.

"Matumizi ya teknolojia pia yataondoa matatizo ya watu kukosa sifa ya kugombea kwa madai kuwa wamechelewa kurudisha fomu kutokana na wahusika kufunga ofisi au kuondoka ofisi lakini sheria kama itaruhusu watu warejeshe fomu kwa njia ya kielektroniki hakutakuwa na shida hiyo tena," alisema.



Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania, Dk. Ananilea Nkya, akiwasilisha maoni ya jukwaa hilo mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria jijini Dodoma jana. Kamati hiyo inaendelea kupokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakuu wa shule wapewa mbinu kuongeza ufaulu

**Na Ibrahim Joseph,** KONDOA

WAKUU wa shule na walimu wakuu katika Halmashauri ya Mji wa Kondoa wametakiwa kufuata miongozo na taratibu wanazopatiwa ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa eneo hilo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Madiwani ya Uchumi, Elimu na Afya, Rachel Sombida, alisema hayo wakati wa kikao cha kuweka mikakati ya kuinua elimu na wakuu wa shule na walimu wakuu kilichofanyika halmashauri ya mji hapa juzi.

Sombida aliwataka wakuu hao kuhakikisha wanazingatia miongozo na mikakati inayowekwa ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi kwenye maeneo yao.

Aliwasihi kufuata taratibu na kuheshimu sheria zote zilizowekwa kwenye maeneo ya shule zao na kujifunza, kujiendeleza kielimu kila wakati na kuwa wabunifu katika kufundisha ili kuinua ufaulu katika shule zao.

Aliwasihi pia kutembelea shule mbalimbali ili kujifunza namna ya ufundishaji na mipangilio mingine wanayofanya huko.

Aidha aliwapongeza walimu wote kwa kazi ya ufundishaji iliyopandisha ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba kutoka asilimia 86.3 mwaka 2022 hadi asilimia 88.4 mwaka 2023.

Mthibiti Ubora Elimu Halmashauri ya Mji Kondoa, Fedrick Moiro, aliwasihi walimu hao kuyafanyia changamoto zinazojitokeza kwenye maeneo yao kazi na kutokatishwa tamaa na wasiopenda maendeleo ya elimu kwenye eneo hilo

Moiro aliwaelekeza pia kuwa na ushikamano katika kazi zao kubadilishana uzoefu katika shughuli mbalimbali wanazofanya ili kukuza taaluma zao na kuandaa vizazi bora kitaaluma.

Katibu wa Tume ya Utumishi ya Walimu (TSC) Halmashauri ya Mji Kondoa, Godfrey Lugano, aliwaelekeza walimu waweke utaratibu wa kufuatilia maadili na taaluma kwa wanafunzi wao. Lugano alisema pia vikao vya wazazi vinatakiwa kufanyika mara kwa mara ili kudhibiti tabia zisizofaa za wanafunzi wao ili kuwajengea utaratibu wa kukemea na tuwafuatilie tabia za wanafunzi na hata walimu wasio na maadili mema.

Aliongeza kuwa tume yao imeendelea kushirikiana na vizuri na walimu na kupunguza malalamiko yanayojitokeza kwa kuandaa vikao vya mara kwa mara na walimu jambo ambalo limewafanya walimu wote kufanya kazi kwa usawa bila kuoneana.



HABARI MBEYA

# Adaiwa kuua mkewe kwa kumnyima tendo la ndoa

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia Juma Kyando (36) mkazi wa mtaa wa Dombwela, wilayani Makete mkoani Njombe kwa tuhuma za kumuua mke wake Tumaini Luvanda (35) kwa kumkata mapanga na kumtenganisha kichwa na kiwiliwili kwa kudaiwa kumnyima tendo la ndoa.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Kamishna Msaidizi, Mahamoud Banga, alisema tukio hilo limetokea juzi saa tisa alasiri ambapo baada ya kufanya tukio hilo alichukuwa baadhi ya viungo na kuvitupa katika mto ulio jirani na nyumba yake eneo la Kabinda.

Kamanda Banga alisema kuwa wanandoa hao walikuwa katika mgogoro wa muda mrefu na sababu ilikuwa ikitajwa kuwa mwanamke hampi unyumba mwanamume.

"Na walijaribu kusuluhisha kwa muda mrefu lakini baadaye ikawa inaonekana mwanamke kama analazimishwa kufanya tendo la ndoa, hatujawa na uhakika inawezekana mwanamke alikuwa na mwanaume pembeni,kwa sababu siku ya tukio mwanamke alichelewa kurudi nyumbani na kukawa na mzozo," alisema Kamanda Banga.

Alisema siku ya tukio inasemekana kuwa mwanaume alimkagua mwanamke na kumkuta na pedi zile za hedhi lakini hakuamini na kuanza kumshambulia baadaye walikuja wananchi wakaamulia.

"Ikaonekana kama ni mtu ambaye anakwenda kuchanganyikiwa kwa sababu alichukuwa panga na kusababisha wananchi waliokuwa pale wote watoweke kwa hiyo ikampa nafasi yeye kufanya tukio hilo," alisema.

Alisemabaada ya jitihada kubwa walimkamata mtuhumiwa katika kanisa lililopo karibu na nyumbani kwake alipokimbilia kwa ajili ya kwenda kuungama.

Awali Mwenyekiti wa mtaa wa Dombwela, Joseph Mbilinyi, alisema alipigiwa simu na jirani kwamba kuna mtu anamshambulia mke wake, alipofika alikuta mtuhumiwa ameshika huku watu wakisita kumsogelea hivyo alipiga simu kwa Jeshi la Polisi kuomba msaada.

"Uwanjani tulikuta moyo wa mtu alimtoa mkewe baada ya kumuua ndio tukaanza kufuata alama za mfuko aliokuwa anavuta mpaka kwenye mto na tukaona kitu kinaelea juu ya maji tukakiopoa.

Pia tukaona viungo vingine kama vile ubavu titi na shingo, tukaanza kutafuta kichwa, hicho ndio kimetusumbua mpaka kukipata maana alitupa sehemu tofauti," alisema Mbilinyi.

Kwa upande wake ndugu wa mtuhumiwa wa mauaji hayo, Medrick Kyando,alisema ndugu yake hana historia ya kuwa na matatizo ya akili lakini anashangaa kuona ametekeleza tukio hilo la kikatili.

"Ndugu yetu hana historia ya tatizo la afya ya akili ni fundi kujenga alikuwa hana makundi na hata tulipopigiwa simu kuhusu tukio hili tulishtuka sana, hebu angalia sasa mama yuko mochwari,baba yuko polisi na watoto wapo watatu ni wadogo sana wataishi mazingira yapi," alisema Kyando.

Baadhi ya majirani walisema kuwa jirani yao alikuwa anaishi vizuri na mke wake na hawajawahi kusikia matukio yoyote ya ajabu lakini wameshangaa kuona ametekeleza tukio la kikatili kama hilo kwa mkewe.

"Wanadamu hatuwezi kujua shida ni nini, hata hatuamini hivi ni kweli? Binadamu gani anatenganisha kila sehemu ya viungo vya mkewe kama mnyama," alisema Jeita Nkwama.



Wakazi wa Kijiji cha Shisyente kilichoko Kata ya Shizuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakishiriki kwenye shughuli ya kuchimba mtaro kwa ajili ya kupitisha bomba la maji ya mradi wa maji wa kijiji hicho unaotekelezwa na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Makambako yajipanga kuanza kufundisha mtaala mpya elimu

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Makambako Mkoa wa Njombe, imesema imejipanga kuhakikisha wanafunzi wa shule za msingi mjini humo wanaanza kufundishwa mtaala mpya wa elimu ambao umeboreshwa katika mwaka wa masomo 2024.

Hayo yalibainishwajuzi na Kaimu Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Mji wa Makambako, Yusto Nyamle, alipotembelea Shule ya Msingi Azimio.

Alisema mtaala huo utakuwa na tija kwa wanafunzi kwa kuwa utawawezesha kujifunza kwa vitendo zaidi badala ya nadharia hivyo kupata uhalisia zaidi wa kile wanachojifunza.

"Kuna uboreshaji wa mtaala mpya utakaogusa awali, darasa la kwanza , la pili mpaka la tatu pamoja na kwamba la tatu wao walikosa baadhi ya vitu walipokuwa kwenye ngazi ya awali la kwanza na la pili, serikali imeagiza wapewe mafunzo ndani ya wiki sita," alisema Nyamle.

Kwa upande wake, Ofisa Elimu Taaluma Sekondari Halmashauri ya Mji wa Makambako, Catherine Ulaya aliwataka viongozi wa serikali ngazi ya mitaa na kata kuhakikisha watoto wote ambao wamechagulia kujiunga na kidato cha kwanza wanaripoti shuleni kwa wakati.

"Tuhakikishe tunasimamia hili zoezi la watoto wote waliochaguliwa kujiunga na sekondari kuripoti shuleni badala ya kukaa huko mitaani au kufanya kazi za nje sehemu nyingine kwa sababu tunapoteza ndoto zao," alisema Ulaya.

Mkuu wa Shule ya Msingi, Azimio Halmashauri ya Mji wa Makambako, Maisha Mhapa alisema mpaka sasa wanafunzi 131 wameanza darasa la kwanza.

"Uandikishaji halisi hadi sasa, wavulana 24, wasichana 32 jumla ni 56 kwa hiyo asilimia ya uandikishaji darasa la awali ni 294 na uandikishaji hadi sasa darasa la kwanza ni 131 ikiwa wavulana 62 na wasichana 69 na hivyo kufanya asilimia ya uandikishaji hadi sasa kuwa ni 108," alisema Mhapa.

Nao baadhi ya wazazi akiwemo, Israel Shedu, alisema wameridhishwa na hali ya miundombinu ya shule na kueleza kuwa watahakikisha wanatekeleza wajibu wao kwa kuchangia chakula.

"Sisi katika shule yetu tumekubaliana mzazi alete mahindi debe mbili na maharage debe moja na fedha Sh. 30,000 kwa ajili ya kumlipa mpishi na kununua kuni," alisema Shedu.

# Najivunia yatoa msaada shule nne zenye walemavu

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SHULE nne za Msingi wilayani Kyela katika mkoa wa Mbeya, zinazofundisha watoto wenye uhitaji maalum, zimepatiwa vifaa vya michezo, kujifunzia na kufundishia ili wasome kwa utulivu na kucheza michezo mbalimbali wawapo shuleni.

Umoja wa kikundi cha Najivuniaunaounganisha wazawa wa wilaya hiyo waishio ndani na nje ya nchi waliungana kwa ajili ya kusaidia shule hizo ambazo ni Mwenge, Sama, Kasumulu na Matemaikiwa ni sehemu ya kurudisha fadhila kwa ndugu zao.

Kwa kutambua mahitaji kwa watoto wenye mahitaji maalum wanaosoma shule maalum za Msingi wilayani Kyela, Umoja wa Najivunia umetoa msaada wa fimbo nyeupe kwa watoto watatu wasioona kwenye shule ya Msingi Mwenge, chati za kusomea kwa watoto wenye uoni hafifu na kengele maalum kwa ajili ya watoto viziwi.

Akikabidhi misaada hiyo juzi, Mwenyekiti wa Jamii wa umoja huo, Vanessa Ngesyenge, alisema misaada hiyo ina thamani ya Sh. milioni 2.5 na kwamba gharama zote zilielekezwa kununua mahitaji ya watoto wenye ulemavu.

Alisema walitoa chati zenye wanyama, matunda na rangi mbalimbali kwa ajili ya kuwavutia watoto hao kufurahia masomo wanayofundishwa na mipira kwa ajili ya michezo wawapo shuleni. "Tulibaini vikwazo vinavyowapata watoto hawa katika shule zetu za msingi, kuna uhaba wa vitendea kazi na miundombinu pia sio rafiki kwao. Kama sehemu ya jamii tumeona tusaidie upande huo lakini bado mahitaji ni makubwa nafikiri wadau wengine waongeze nguvu.," alisema Vanessa.

Akizungumza kwa niaba ya serikali, Ofisa Elimu ya Watu Wazima naElimu Nje ya Mfumo Rasmi, Geofrey Paul, alisema wanawahudumia watoto wenye usonji, viziwi na wenye matatizo ya akili ambao wanahitaji uangalizi wa karibu huduma bora na mazingira mazuri ya kusoma.

Alisema bado wanahitaji msaada ya hali na mali kuwasaidia watoto hao vikiwemo vifaa vya kujifunzia kama chati nundi, fimbo nyeupe, viti mwendo, vifaa vya michezo, madarasa yenye picha na muonekano ambao utawavutia watoto hao na kupenda kusoma kuliko ilivyo sasa ambapo bado mazingira sio rafiki.

Msemaji wa Umoja huo, Lwitiko Mwangoka, alisema wamebaini mahitaji kwa watoto hao wataendelea kutoa michango ya hali na mali ili wasome kwa utulivu na kutimiza ndoto zao.



# Barabara za juu kuboresha uchumi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya ujenzi ya China (CCECC), imesema miradi ya ujenzi ya Barabara inayoendelea Zanzibar ikiwemo barabara za juu (Fly Over) itasaidia kukuza uchumi na kubadilisha mwonekano wa mazingira ya Zanzibar ambao ni mji wa kitalii.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo Zhang Junle alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari visiwani Zanzibar kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara za ndani ya mji wa Zanzibar ambao unatarajiwa kugharimu zaidi ya Shilingi bilioni 232.

Alisema ujenzi wa Barabara ya uwanja wa ndege hadi Mnazi mmoja yenye urefu wa kilomita 6.5 umekamilika na ule wa barabara ya juu unaendelea kufanyika katika eneo la Mwanakwerekwe.

Akizungumzia uzoefu wa kampuni yake, alisema inauwezo mkubwa wa kujenga barabara zenye kiwango cha ubora na imekuwa ikitekeleza miradi kama hiyo katika maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki.

Alisema kampuni hiyo pia imefanikiwa katika ujenzi wa reli ya Tazara ambayo inaihusisha Tanzania na Zambia.

Alisema kwa upande wa Zanzibar barabara walizojenga ni ya Mkokotoni hadi Mtoni yenye urefu wa kilomita 52 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

Alisema serikali ya mapinduzi ya Zanzibar inatarajia kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 277 kupitia shirika hilo na shughuli za ujenzi zinaendelea katika barabara mbalimbali Zanzibar.

Alisema mpaka sasa wananchi 960 wamenufaika na miradi wanayoendelea kuitekeleza zikiwemo kutoa ujuzi, kuwajengea uwezo na kutengeneza maeneo ya barabara yanayokabiliwa na uchakavu.

Junle alipongeza serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufikisha miaka 60 ya mapinduzi huku ikiendelea kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kuwasogezea maendeleo wananchi wake na kujenga misingi ya amani na umoja wa kitaifa.

Aidha alisema kumbukumbu za historia zinaonesha Zanzibar na China zimekuwa na ushirikiano wa muda mrefu tangu kufanyika kwa mapinduzi mwaka 1964 na ipo miradi mingi ya kihistoria iliyofadhiliwa na China, misaada ya wataalamu wa tiba katika kuendeleza malengo ya mapinduzi ya Zanzibar.

Mkuu wa mradi wa kampuni hiyo, Xiong Yun Xu, alisema utekelezaji wa miradi ya barabara zinazotakiwa kujengwa Zanzibar unaendelea vizuri na tayari barabara ya Uwanja wa ndege hadi mnazi mmoja imezinduliwa na Rais Dk Mwinyi ambayo imejengwa na kampuni hiyo.

Aidha alisema mabadiliko ya hali ya hewa ikiwemo mvua za amino zilizojitokeza imekuwa changamoto kubwa katika shughuli za ujenzi lakini wanakabiliana nazo ili kuhakikisha kasi ya ujenzi inaendelea kufanyika.

# Bei ya mafuta ya petroli yashuka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BEI ya mafuta kwa Mwezi wa Januari imeshuka Zanzibar, sababu ya kushuka kwa bei hiyo ikielezwa kuwa ni kushuka kwa gharama za mafuta katika soko la dunia na za uingiaji wa mafuta.

Akitangaza bei hizo, jana Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbarouk Makame Haji, alisema Petroli kwa mwezi huu lita moja inauzwa Sh.2,893 kutoa Sh. 2,910 ya mwezi Desemba ikiwa ni tofauti ya asilimia 0.58.

Alisema bei ya Dizeli kwa mwezi huu ni 3,101 wakati Desemba iliuzwa Sh, 3,168 ikiwa ni tofauti ya asilimia 2.12 huku mafuta ya taa yatauzwa Sh. 3,200 kutoka Sh. 3,300 ya Desemba mwaka jana, tofauti ya asilimia 3.03.

Aidha alisema bei ya mafuta ya ndege kwa mwezi huu ni sh.2,825 ikilinganishwa na Desemba mwaka jana ambayo ilikuwa ni sh. 2,973 tofauti ya asilimia 4.98.

Alisema mamlaka hiyo hupanga bei kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani na gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam na Tanga.

Alisema pia wanazingatia thamani ya shilingi ya Tanzania kwa dola ya kimarekani, gharama za usafiri, bima, kodi na tozo serikalini.

"Kodi na tozo za serikali, kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na reja reja nazo ni miongoni mwa mambo tunayoangalia tunapopanga bei za mafuta"alisema.

Hata hivyo aliendelea kuwasihi wananchi kununua mafuta katika vituo halali sambamba na kudai risiti za kielektroniki.



Wanafunzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Tumekuja wakiwa katika chumba cha maabara wakati Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), alipotembelea madarasa mbalimbali baada ya kuifungua, iliyojengwa Mwembeladu Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali yavuka lengo ujenzi wa barabara

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imevuka lengo la ujenzi wa barabara visiwani kwa kujenga yenye urefu wa kilomita 500 likizidi lililoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambalo ni kilometa 200. Akizungumza juzi wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara ya kilomita 6.5 ya Uwanja wa Ndege wa Kiembesamaki hadi Mnazi Mmoja Wilaya ya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi, Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, alisema Serikali inajenga mtandao wa barabara za kilomita 100 mijini kwa Unguja na Pemba.

Alisema pia imejenga barabara zenye urefu wa kilomita 130 kati ya Tunguu-Makunduchi, Kisauni - Fumba na Chake - Mkoani, Pemba mbali na barabara za kilomita 285 za vijijini.

Rais Dk. Mwinyi alisema, barabara hizo zinategemewa kudumu kwa zaidi ya miaka 50 hadi 70 ijayo kutokana na uimara na ubora wa kiwango cha hali ya juu uliojumuishwa na miundombinu ya kupishia maji ikiwemo mitaro ya maji machafu.

Akizungumzia adha za usafiri wa umma nchini, Rais Dk. Mwinyi alisema, serikali imedhamiria kuondosha changamoto ya foleni barabarani na usumbufu kwa wananchi ikiwemo ujenzi wa barabara za juu Amani - Mwanakwerekwe.

Rais Dk. Mwinyi pia alisema, serikali yake imekusudia kuweka usafiri wa umma wa uhakika ili kuwaondolea wananchi wake usumbufu kwa kuleta mabasi ya kisasa yatakayokidhi haja za wananchi.

Alisema pia serikali ina mpango wa kuweka usafiri wa umma utakaotumia gesi na umeme na kudhibiti changamoto zinazosababishwa na usafiri huo kwa kuendelea kujenga vituo vingi vya mabasi ya usafiri wa umma.

Pia Rais Dk. Mwinyi aliwasisitiza wananchi kuzitumia vizuri barabara hizo kwa kukuza uchumi wa nchi sio kusababisha maafa na ajali kwa kujiepusha na uvunjifu wa sheria barabarani na kuepuka mwendo wa kasi.

Aidha, aliviomba vyombo vya usalama barabarani kuwachukulia hatua kali za sheria madereva na watumiaji wa barabara hizo watakaokwenda kinyume na sheria.

Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed alisema, Serikali imekusudia kurejesha historia ya Zanzibar ya mwaka 1879 ya usafiri wa umma wa treni kama iliyotoka Mji mkongwe hadi Chukwani na ile ya mjini hadi Bububu.

Alisema Serikali itajenga miundombinu ya kisasa ya usafiri treni za abiria pamoja na kuweka mfumo mpya wa mabasi ya umeme kwa maagizo ya Rais Dk. Mwinyi.

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Khadija Khamis Rajab alisema, ujenzi wa barabara ya Uwanja wa ndege Mnazi mmoja yenye urefu wa kilomita 6.5 umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 5, ina upana wa mita saba kila upande na uwezo wa kupitisha magari yenye uzito wa 50.

Alisema barabara hiyo yenye ubora wa kiwango cha G45, imejumuisha mitaro kila upande, pamoja na madaraja madogo 41 yatakayopitisha miundominu ya huduma za jamii ikiwemo miundominu ya maji, umeme na mawasiliano, taa za barabarani na taa za kuongozea magari.

Akizungumza kuhusu fidia kwa wananchi walioathiriwa na barabara hiyo, Katibu Khadija alisema, hakuna fidia yoyote iliyogharimu Serikali kwa ujenzi wa barabara hiyo isipokuwa wananchi wawili ambao tayari washafanyiwa tathmini baada ya kuonekana kuna haja ya wao kupisha ujenzi wa barabara hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANTHONY MRUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P0308-0123 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ENABOISHU SEKONDARY SCHOOL CENTRE** mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/54092/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASIFIWE DEUS NDAYISHALIYE** anatangaza kupotelewa na Kadi ya gari aina ya MITSHUBISHI CANTER, yenye usajili NAMBA T372 AQG. CHASSIS NAMBA FE435E541986 na ENGINE NAMBA 4D33804067. Yeyote atakayeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye. Taarifa ya Polisi: **MWA/NYA/RB/166136/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DIANA YOHANA MARWA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T994EFF AINA YA SUBARU FORESTER, RANGI NYEUSI YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA

**PHQ/IRI/IRI/427/2024..**

---

**FOMU MIRATHI**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na. 80/2022**

**FABIAN NGOLE:::::::::::::::::::::Marehemu**
**SOPHIA FABIAN NGOLE:::::::::::::::Mwombaji**

### TAARIFA KWA WADAI

**(Kanuni ya 9 (1) ya Nyongeza ya V ya Sheria ya Mahakimu wa Mahakama Sura ya 11 Rejeo la 2019)**

TAARIFA inatolewa hapa kwa wote wanaodai kuwa na madai yanayohusiana na mali za marehemu mtajwa hapo juu FABIAN NGOLE, aliyefia Lunyanywi, tarehe 23 mwezi wa 10 mwaka 2023, na Mahakama kunipa barua ya usimamizi wa mirathi hiyo mimi SOPHIA FABIAN NGOLE siku ya tarehe 24 mwezi wa 11 mwaka 2023, hapa sasa wanatakiwa kunipa madai yao kwangu kupitia sanduku langu la barua 54 Njombe au namba ya simu 0745699102, au kuniletea kwa binafsi, ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangazwa taarifa hii ambapo muda wake utapoisha nitaendelea kukabidhi mali za marehemu kwa warithi wanaostahili, nikizingatia tu madai ambayo kwayo nitakuwa nimearifiwa.

Sophia Fabian Ngole

Imepitishwa na itangazwe Gazetini na ofisi za mlaa

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na....1888../2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SAID ABDALLAH WA........................**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA RAMADHANI SAIDI KING'OMA**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 05 Mwezi 02 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 01 mwaka 2024

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...4/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: MWANABARAKA AHMED AMEIRY wa MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA FRANK SIXBERT HAULE**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 1 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 9 mwezi 1 mwaka 2024

HAKIMU
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO
MOROGORO

---

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**AT SAMORA AVENUE**
**COMMERCIAL CIVIL CASE NO. 05/2023**
**BANK OF AFRICA (T) LTD......PLAINTIFF**
**VERSUS**
**JESSE MUTALEMWA RUMANYISA......DEFENDANT**

**TO: JESSE MUTALEMWA RUMANYISA**
**P.O. 25**
**BUKOBA**
Take notice that the plaintiff has instituted a suit against you with particulars of claim set out in a plaint filed in this court.
Service of the summons on you has been ordered by means of this publication. You are defected to collect copies of the summons and plaint from the court's registry.
You are hereby summoned to appear in this court in person or by an advocate or an agent duly authorized on 01-02-2024 at 8:30 a.m when this suit will be mentioned.
Take further notice that should you default to enter appearance in court on the day time mentioned above, the suit will proceed and judgment may be given in your absence.
Given under my hand the seal of the Court this day of 4-01-2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT ILALA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 18 OF 2024**
**In the matter of the Estate of the late GERALD SIMON MSENGA of Mapinduzi North, Dodoma Makulu Ward within Dodoma City Council**
**And**
**In the matter of application for Letters of administration by ROSE GERALD MSENGA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of 1..................... 2024
Dated at Dodoma this 09 Day of 1...2024...PETITIONER
Presented for filing this 9... Day of 12024

RESIDENT MAGISTRATE

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARIKIMATAIFA

# Daglo atuhumiwa kuhusika na uhalifu wa kivita Sudan

**KHARTOUM, Sudan**

KIONGOZI wa kikosi cha wanamgambo wa (RFS) nchini Sudan Mohamed Daglo anatuhumiwa kuhusika na uhalifu wa kivita nchini humo, wakati akiendeleza ziara yake kwa mataifa ya kikanda ili kutafuta uungwaji mkono.

Ilielezwa kuwa Daglo amekua akifanya safari za kikanda ikiwa ni juhudi za kujaribu kutafuta uungwaji mkono na viongozi wa kikanda na bara la Afrika, pamoja na kujaribu kusuluhisha mzozo ambao umesababisha vita kati ya kikosi chake na jeshi la Sudan.

Ilibainishwa kuwa Daglo alifanya mazungumzo na marais wa Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Rwanda, na Djibouti pamoja na Ethiopia, ili kutafuta njia mwafaka ya kumaliza mzozo na kwamba mchakato wa amani unaoendelezwa nchini humo, unastahili kufikia suluhu ya kisiasa itakayoleta amani ya kudumu katika taifa hilo, ambalo kiongozi huyo anapata ungwaji mkono kutoka utawala wa Chad.

Inaelezwa kuwa kiongozi wa utawala wa kijeshi nchini Sudan, Abdel Al-Burhan naye alionekana kupata ungwaji mkono kutoka kwa taifa la Misri na Eritrea.


Aidha, ilielezwa kuwa hivi karibuni wapiganaji wa RSF nchini Sudan wameonesha utayari wao wa kusitisha mara moja mapigano na bila masharti yoyote kupitia mchakato wa mazungumzo na Jeshi la Sudan.

Vita nchini Sudan vilivyoanza mwezi Aprili 2023, na kutajwa kusababisha vifo vya zaidi ya watu 12,000 huku Umoja wa Mataifa ukisema kuwa zaidi ya watu milioni 7 wameyakimbia makazi yao.

Hata hivyo, Tume ya Umoja wa Mataifa nchini Sudan Kusini, (UNMISS), ililaani vurugu zilizosababisha vifo vya raia 28 kwenye mji wa Dukar, kaunti ya Jonglei.

Ilielezwa kuwa UNMISS sasa inawataka viongozi wa eneo la Jonglei na Pibor, kukutana kwa mazungumzo ili kuepuka mashambulio ya ulipizaji kisasi baada ya vijana wa Murle kutekeleza mauaji hayo.

**RFI**



Mkuu wa Kikosi cha Msaada wa Haraka (RSF) nchini Sudan, Mohamed Daglo (kushoto), akizungumza na Rais wa Kenya Wiliam Ruto. **PICHA MTANDAO.**

# Korea Kusini yapiga marufuku biashara ya nyama ya mbwa

**SEOUL, Korea Kusini**

KOREA Kusini imepitisha sheria mpya, ambayo inalenga kukomesha uchinjaji na uuzaji wa nyama ya mbwa kama moja ya sehemu ya biashara ya chakula nchini humo ifikapo 2027.

Ilielezwa kuwa sheria hiyo inalenga kukomesha tabia ya karne nyingi ya kula nyama ya mbwa. Na kwamba kwa sasa nchini humo imekosa kupendwa na watu wengi hasa vijana.

Pia inabainishwa kuwa chini ya sheria hiyo, kufuga au kuchinja mbwa kwa ajili ya kuliwa kutapigwa marufuku,pamoja na kusambaza au kuuza nyama ya mbwa. Na kwamba wale watakaopatikana na hatia ya kufanya hivyo watachukuliwa hatua ikiwemo kuhukumiwa kifungo cha gerezani. Aidha ilielezwa kuwa wale wanaochinja mbwa wanaweza kufungwa jela miaka mitatu, huku wale wanaofuga kwa ajili ya kuuza nyama ya mbwa wanaweza kutumikia kifungo cha miaka miwili.

Hata hivyo, licha ya adhabu hizo zitakazochukuliwa kwa wauzaji na wafugaji wa mbwa kwa ajili ya nyama, inaelezwa kuwa ulaji wa nyama ya mbwa yenyewe hautakuwa kinyume cha sheria.

Vile vile, inaelezwa kuwa sheria hiyo mpya itaanza kutumika miaka mitatu ijayo, na kuwapa wakulima na wamiliki wa migahawa muda wa kutafuta vyanzo mbadala vya ajira na mapato. Pia inatajwa kuwa watalazimika kuwasilisha mpango wa kumaliza biashara zao kwa mamlaka zao za mitaa.

Kadhalika inaelezwa kuwa serikali nchini Korea Kusini iliahidi kusaidia kikamilifu wakulima wa nyama ya mbwa, wachinjaji na wamiliki wa migahawa, ambao biashara zao zitalazimika kufungwa, ingawa maelezo ya iwapo fidia itatolewa bado hayajafanyiwa kazi.

Kwa mujibu wa takwimu za serikali, Korea Kusini ilikuwa na karibu migahawa 1,600 ya nyama ya mbwa na mashamba 1,150 ya mbwa mnamo 2023.

Kitoweo cha nyama ya mbwa, kinachoitwa boshintang, kinachukuliwa kuwa kitamu miongoni mwa baadhi ya Wakorea Kusini wenye umri wa juu, lakini nyama hiyo si maarufu tena kwa vijana.

**BBC**

## Mtoto wa rais aliyepinduliwa Niger aachiwa

**NIAMEY, Niger**

UTAWALA wa kijeshi nchini Niger umemuachia huru kwa muda mtoto wa Rais aliyepinduliwa madarakani Mohamed Bazoum, Salem Bazoum huku mahakama ya kijeshi ikieleza kuwa atatakiwa kuwasili mahakamani ikiwa atahitajika.

Chanzo kilicho karibu na Rais Bazoum kimeliambia shirika la habari la AFP kwamba Salem Bazoum aliondoka Mjini Niamey kuelekea Lome, mji mkuu wa Togo.

Togo ni miongoni mwa mataifa kadhaa ya Afrika Magharibi ambayo yamehusika katika upatanishi na utawala wa kijeshi wa Niger. Na kwamba licha ya vikwazo mbalimbali imeendelea kuwa na uhusiano wa karibu na Niger.

Kwa mujibu wa televisheni ya umma ya Niger, Waziri wa Mambo ya Nje wa Togo Robert Dussey alikuwa ziarani mjini Niamey, na kukutana na waziri mkuu.

Inaelezwa kuwa tangu mapinduzi ya Julai 26, 2023 Niger inatawaliwa na viongozi wa jeshi na Rais Bazoum na familia yake wanaendelea kuzuiliwa katika makazi ya rais.

Mapinduzi hayo yalilaaniwa kimataifa huku taifa hilo likikabiliwa na matatizo ya kiuchumi kutokana na vikwazo vya Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS).

Bei ya vyakula imepanda na kumeshuhudiwa uhaba wa bidhaa muhimu kama vile dawa, katika moja ya nchi maskini zaidi duniani.

Hata hivyo, mtawala wa kijeshi Jenerali Abdourahamane Tiani alisema ataongoza serikali ya mpito kwa muda wa miaka mitatu kabla ya kurejesha serikali ya kiraia.

Utawala mpya wa kijeshi nchini Niger umejitenga na washirika wake wa jadi wa mataifa ya Magharibi hasa Ufaransa, na umekuwa na mahusiano ya karibu na majirani zake wawili, ambao ni Mali na Burkina Faso, ambazo pia kwa sasa zinaongozwa na wanajeshi baada ya mapinduzi.

Wanajeshi wa mwisho wa Ufaransa waliondoka Niger Desemba 2023. Kama ilivyo kwa nchi jirani za Burkina Faso na Mali, na kwamba Niger inakabiliwa pia na uasi wa makundi ya kigaidi hasa katika eneo ambalo nchi hizo tatu za Sahel zinapakana.

Siku chache zilizopita, Rais wa Benin Patrice Talon alitoa wito wa kuanzishwa upya na kwa haraka uhusiano kati ya nchi yake na Niger. Na kwamba wiki moja baadaye Benin iliondoa vikwazo kwa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje zinazopitia Niger kupitia bandari ya Cotonou baada ya miezi mitano ya vikwazo.

Kwa sasa uanachama wa Niger bado umesimamishwa katika Jumuiya ya ECOWAS, ambayo ilisema kuachiliwa kwa Bazoum na kurejea kwake madarakani ni miongoni mwa masharti ya kulegezewa vikwazo.

**DW**

# BALUA AFUNGUKA KUHUSU KUTUA KUITUMIKIA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya tetesi za muda mrefu zinazomhusu winga wa Prisons, Edwin Balua kujiunga na klabu ya Simba, hatimaye mwenyewe ameibuka na kusema kama atakwenda huko litakuwa ni jambo jema na yupo tayari kuzikabili changamoto zozote atakazokutana nazo.

Kwa muda mrefu mchezaji huyo anayecheza winga zote mbili, huku akiwa kwenye kiwango cha juu msimu huu, akiwa ameshapachika mabao mawili amesema pamoja na yote hayo, kila kitu kiko kwa viongozi wake ambao ndiyo watamwambia nini cha kufanya.

"Nadhani kila kitu kipo kwa uongozi wangu kama kutakuwa na mazungumzo yoyote juu ya hilo, wenyewe ndio watanifahamisha," alisema Balua.

Zipo taarifa kuwa viongozi wa Simba wanamalizana kwanza na uongozi wa Prisons kwa ajili ya kulipa pesa ili kuvunja mkataba uliopo kati ya mchezaji wa Maafande hao ili kila kitu kiwe wazi.

Imeelezwa kwa sasa mchezaji huyo hawezi kuongea lolote kama amekuwa na mazungumzo na Simba au la kwa sababu mkataba haumruhusu na itaonekana klabu imezungumza na mchezaji wakati akiwa kwenye mkataba na klabu nyingine.

Alipoulizwa kama atajiunga na Simba, alisema litakuwa ni jambo jema kwake kwani yeye pia ni mchezaji mwenye ndoto za kwenda juu zaidi.

"Kwanza ni jambo jema na kama itatokea mimi ni mchezaji, changamoto yoyote inaweza kunitokea na naweza kufanya kazi katika timu yoyote ile hata iwe kubwa," alisema Balua ambaye alifunga bao la kufutia machozi kwa mkwaju wa faulo, Oktoba 5, mwaka jana, Prisons ikipokea kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa Simba katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Kama akisajiliwa atakuwa ni mcheza wa nne kipindi hiki cha dirisha dogo, baada ya Salehe Karabaka kutoka JKU, Babacar Sarr mchezaji huru na Ladack Chasambi kutoka Mtibwa Sugar.

# Pwani sasa yataka timu Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

MKOA wa Pwani umeanza kampeni kabambe wa kuhakikisha unarudisha timu zake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya Ruvu Shooting kuteremka msimu uliopita.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Chama cha Soka Mkoa wa Pwani (CORREFA), Christina Mwagala, amesema kuteremka daraja kwa Ruvu Shooting ni moja ya changamoto ambazo wamekutana nazo, hivyo sasa kulazimika kuandaa mikakati ya kuzisapoti timu mbili za Kiluvya FC na Nyumbu FC ili kufanya vizuri, hatimaye kuziona zikiwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Mkakati wa COREFA ni kuzipandisha timu kwa sababu hivi sasa hatuna timu ya Ligi Kuu, Ruvu Shooting ambayo ipo Championship imeshahama mkoa, hivi sasa tuna Nyumbu na Kiluvya FC zinazocheza 'First League,' ambayo kingazi ni Ligi Daraja la Pili.

Tunaangalia namna ya kuzisapoti timu hizi ili zipande, Pwani hatustahili kuwa mkoa ambao hauna timu ya Ligi Kuu, ni upepo mbaya tu ulijitokeza mpaka Ruvu Shooting ikashuka daraja ili kwenye mkoa wetu, na hii ni moja kati ya changamoto tuliyoichukua, katika uongozi huu wa Mwenyekiti Robert Munisi tutahakikisha mambo yanakaa sawa," alisema Mwagala.

Timu hizo mbili zote zipo Kundi A, kwenye First League, ambalo kwa sasa linaongozwa na African Sports yenye pointi 14, huku timu za Mkoa wa Pwani, Nyumbu FC na Kilunya FC zikiwa kwenye nafasi ya tatu na nne kila timu ikicheza mechi sita.

Nyumbu FC ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi 10, ikicheza mechi sita, ikishinda tatu, sare moja na kupoteza moja, huku Kiluvya FC ikiwa nafasi ya nne ikiwa na pointi tisa, ikishinda mechi mbili, sare tatu na kupoteza moja.




Winga wa Azam FC, Kipre Junior, akiambaa na mpira dhidi ya kiungo wa Singida Fountain Gate kwenye mechi ya hatua ya robo fainali ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa katika Uwanja wa New Amaan Sports Complex, visiwani Zanzibar juzi. Singida FG ilishinda mabao 2-1. **MPIGAPICHA WETU**

# Ndumbaro awaita wadau kuchangia timu zote za taifa

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, amewaomba wadau wa sekta mbalimbali kuziunga mkono timu za taifa za michezo mbalimbali kwa kuwa serikali peke yake haitaweza kuzihudumia.

Wadau hao wameombwa kuanza kuchangia katika harambee inayozinduliwa rasmi jijini Dar es Salaam.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kushiriki kwa njia ya mtandao, lakini Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, atamwakilisha katika harambee hiyo ya kuchangia timu za taifa ambazo zinaenda katika mashindano mbalimbali kwa mwaka huu wa 2024.

Akizungumza na Nipashe jana, Waziri Ndumbaro, alisema kunahitajika mchango wa wadau wengine kwani kutokana na wingi wa michezo nchini, kuna timu zaidi ya 20 za taifa katika michezo mbalimbali.

Alisema harambee itakayofanyika leo ya kukusanya fedha ni utekelezaji wa malengo ya Rais Samia kwa ajili ya kusaidia timu za taifa inayojiandaa na mashindano ya kimataifa, ikiwamo Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) kwa Taifa Stars na Wafcon kwa Twiga Stars.

"Pia kuna mashindano ya All Afrika Games yanayotarajiwa kuanza kati ya Februari au Machi, michuano hiyo Tanzania inaenda kushiriki michezo tisa, hivyo kuna timu tisa za taifa zinaenda kushiriki, ikiwamo Timu ya Soka ya Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors) na Olimpiki nchini Paris huku tunapeleka timu tatu, riadha, ngumi na soka kwa wanawake," alisema Dk. Ndumbaro.

Aliongeza kuwa kamatii ya hamasa aliyoiteua itafanya kazi kwa kipindi cha mwaka mmoja kuhakikisha inakusanya fedha kwa ajili ya kuzihudumia timu za taifa ambazo kwenye soka zipo 10, sita wanaume, nne wanawake, Tembo Warriors na netball iliyoshindwa kusafiri kwenda Botswana.



a

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### JARRAD ATAKIWA MADRID
REAL Madrid inamfuatilia beki wa kati wa Everton na England mwenye umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite. **(Mail)**

### ONANA AITAKA ARSENAL
KIUNGO wa kati wa Everton na Ubelgiji, Amadou Onana mwenye umri wa miaka 22, anataka kuhamia Arsenal. **(Sacha Tavolieri)**

### DAVID AWINDWA EPL
MANCHESTER United na Aston Villa zinataka kumsajili mshambuliaji wa Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 23 kutoka Lille. **(Football Transfers)**

### CARVALHO KWA MKOPO
KIUNGO wa kati wa Liverpool na Ureno, Fabio Carvalho mwenye umri wa miaka 21, anatazamiwa kujiunga na Hull City kwa mkopo kwa muda uliosalia wa msimu huu. **(Mail)**

### HENDERSON KUTOACHIWA
KLABU ya Saudi Arabia, Al-Ettifaq haitaki kumpoteza kiungo wa kati wa England, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 33, mwezi huu na bado haijapokea ofa rasmi au isiyo rasmi. **(Ben Jacobs)**

### PHILLIPS NA NEWCASTLE
MAZUNGUMZO yanaendelea kati ya Manchester City na Newcastle United kuhusu usajili wa kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, 28. **(Rudy Galetti)**

### BERGWIJN ATAJWA WEST HAM
KLABU ya West Ham itachunguza uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa zamani wa Tottenham Hotspur, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 26, ambaye kwa sasa anachezea Ajax. **(Evening Standard)**

### EKITIKE AIVUTIA WOLVES
KLABU ya Wolves inavutiwa na fowadi wa Paris St-Germain, Mfaransa Hugo Ekitike, 21. **(L'Equipe)**

### PELLISTRI ANUKIA PSV
KLABU ya PSV Eindhoven imeonesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Uruguay, Facundo Pellistri mwenye umri wa miaka 22, kutoka Manchester United. **(Fabrizio Romano)**

### DRAGUSIN ANYATIWA BAYERN
KLABU ya Bayern Munich imeungana na Tottenham Hotspur katika harakati za kumsajili beki wa Romania na Genoa, Radu Dragusin, 21. **(GSP)**

### SPENCE AREJEA SPURS
MLINZI wa kulia Mwingereza, Djed Spence mwenye umri wa miaka 23, anafanya mazoezi na vijana wa Tottenham Hotspur walio chini ya umri wa miaka 21 na anaonekana kurejea kwa mkopo baada ya kutoka Leeds United mwezi huu. **(Football London)**




## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE SASA KUAMUA MUSTAKABALI WAKE PSG

●●● Real Madrid, Liverpool zatajwa huku ikielezwa anavutiwa kuwa chini ya Klopp, lakini...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, ataamua mustakabali wake katika wiki chache zijazo, huku Real Madrid na Liverpool zikiwa ndio sehemu anazoweza kwenda endapo ataamua kuondoka katika mji mkuu wa Ufaransa, kwa mujibu wa ESPN.

Mkataba wa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa katika Klabu ya PSG unamalizika Juni na hautaanzisha chaguo lake la kuongezewa mwaka mmoja, kumaanisha kuwa yuko huru kuzungumza na klabu nyingine kuhusu uhamisho wa majira ya joto.

Real Madrid bado wana nia kubwa zaidi ya kuwania saini yake, huku klabu hiyo ikiwa imejaribu mara kadhaa kumsajili tangu akiwa na umri wa miaka 11, ikikaribia zaidi Mei 2022 waliposhawishika kuwa amekubali kujiunga kabla ya kuamua kubaki Paris.

Licha ya ripoti nchini Ufaransa Jumatatu ikisema kwamba Mbappe amekubali kujiunga na Madrid, vyanzo vya ESPN vimesema bado hawajafikia mwafaka, na kwamba bado kuna mawasiliano kati ya pande hizo mbili.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Mbappe kwa muda mrefu amekuwa akivutiwa na Liverpool na Jurgen Klopp na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 25, hajakataa kuondoa uwezekano wa kuhamia Ligi Kuu England.

Hata hivyo, uhamisho wa kwenda Liverpool unaweza kuwa mgumu kutokana na mshahara mkubwa anaolipwa kwa wiki wa euro 650,000.

Vyanzo viliongeza kwamba Mbappe anaweza kukubali fedha kidogo katika mkataba wake ujao ikiwa ataondoka PSG.

Uwezekano wowote wa kuhama unaweza kuangazia mustakabali wa Mohamed Salah, ambaye alikuwa chini ya ofa kutoka Saudi Pro League msimu uliopita wa majira ya joto, ingawa Mbappe ana nia ya kuamua mustakabali wake hivi karibuni, ikimaanisha kuwa wakati unaweza pia kuwa kikwazo kikubwa.

PSG imebakia kuwa na nia kubwa ya kumbakisha Mbappe, ambaye ndiye mfungaji bora wa klabu hiyo, lakini imekubali kutolipa bonasi kubwa ya uaminifu ya karibu euro milioni 80 iwapo ataondoka.

# DE BRUYNE AFURAHIA KUREJEA UPYA

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa Manchester City, Kevin De Bruyne, amesema mapumziko yake ya miezi mitano kutokana na majeraha yanaweza kuwa baraka kwake na kwa klabu yake.

De Bruyne alirejea kutoka kwa upasuaji wa misuli ya paja katika ushindi wa 5-0 dhidi ya Huddersfield Town Jumapili akiwa hajacheza kikosi cha Pep Guardiola tangu Agosti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye alitoa asisti kwa bao la Jeremy Doku dakika 17 tu baada ya kuingia uwanjani, alisema anahisi kuwa fiti baada ya kukaa nje ya uwanja na yuko tayari kuisaidia City kushinda mataji katika kipindi cha pili cha msimu.

„Sio kama nilihitaji mapumziko lakini ilikuwa ni kama kubadilisha hasara kuwa faida,“ alisema De Bruyne.

„Ninapotafakari kazi yangu, nikicheza miaka 10 iliyopita bila kukoma na mapumziko mafupi, labda ilikuwa nzuri kwangu kuanza upya.

„Nilitumaini ningeweza kufanya kazi kwa bidii na kurudi kwa njia nzuri na ninahisi kuwa ninafanya hivyo, lakini ni wazi nahitaji kuendelea.“

De Bruyne alikosa michezo 27 kabla ya kurejea kwenye kikosi kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Sheffield United mnamo Desemba 30, mwaka jana.

Alipata dakika zake za kwanza dhidi ya Huddersfield na baadaye akakiri ilikuwa vema kurejea, ikiwa tu kwa sababu yeye si shabiki wa kutazama michezo kwenye TV.

„Naweza kutazama soka lolote na nilitazama kila mechi, lakini sipendi,“ alisema.

„Ni wazi wamekuwa sawa. Baada ya mwaka tuliokuwa nao mwaka jana kutakuwa na kupanda na kushuka, lakini michezo mingi isipokuwa Aston Villa na labda Wolves tulifanya vizuri. Tupo na timu zingine.

„Ikiwa uko hapa na timu zote zinazokuzunguka hautakuwa mbali. Tupo pale tunapohitaji kuwa, lakini tunahitaji kujaribu na kuendeleza hilo.“




# Kimmich kusubiri hadi majira ya joto

**MUNICH, Ujerumani**

MANCHESTER City imepanga kusubiri hadi dirisha lijalo la majira ya joto ili kumsajili kiungo wa Bayern Munich na Ujerumani, Joshua Kimmich, ambapo inaamini itampata kwa fedha ndogo.

Kimmich ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2025, mwisho wa msimu huu huenda akauzwa kwa fedha kiduchu zaidi ya ilivyo sasa.

Man City walihitaji kumsajili Kimmich kwenye dirisha hili, lakini inaonekana kuwa ngumu kwa mabosi wa Munich kukubali kumuachia kutokana na umuhimu wake kwenye timu.

Taarifa za awali zilidai kwamba Man City huenda ikawasilisha ofa ya zaidi ya pauni milioni 44 kwa ajili ya kumnasa nyota huyu mwenye umri wa miaka 28, lakini inaaminika msimu ujao huenda bei hiyo ikapungua zaidi.

Matumaini ya kuipata saini yake yanaonekana kuwa makubwa zaidi kwa sababu ya uhusiano kati ya timu hizo mbili zilizofundishwa na Pep Guardiola.






# Adebayor amtaka Osimhen akacheze EPL

**LONDON, England**

NYOTA wa zamani wa Arsenal na Manchester City, Emmanuel Adebayor amesema anaamini Victor Osimhen atafanya vizuri katika Ligi Kuu England (EPL), kama atajiunga nayo.

Osimhen amekuwa akitamaniwa na timu nyingi zinazoshiriki EPL kutokana na uwezo wake wa kufumania nyavu, ambao amekuwa akiuonesha katika kikosi cha Napoli anakocheza hivi sasa.

Klabu za Chelsea, Manchester United na Arsenal zimekuwa zikimtaka mshambuliaji huyo na Adebayor anaamini kama nyota huyo wa Nigeria atajiunga na mojawapo ya timu hizo.

"Ana haiba sahihi na ari ya hatua kule (England). Ninaombea ahamie katika Ligi Kuu England na aonyeshe kile kilicho ndani ya uwezo wake," alisema Adebayor.

Osimhen mwenye umri wa miaka 25, msimu uliopita ndiye alikuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Italia kutokana na mabao yake 26 aliyoifungia Napoli.

HABARI MICHEZO

# YANGA PRINCESS, SINGIDA FG PRINCESS NI VITA LEO

**Na Saad Akida**

KIKOSI cha Singida Fountain Gate Princess leo kitashuka katika uwanja wake wa nyumbani wa Jamhuri jijini Dodoma kuikaribisha Yanga Princess katika mchezo wa raundi ya nne wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara.

Timu hizo zinakutana mara ya pili baada ya mechi ya kwanza Desemba 12, mwaka jana kwenye Ngao ya Jamii kutafuta mshindi wa tatu na Yanga Princess kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-2 baada ya matokeo ya suluhu ndani ya dakika 90, mechi ikipigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Yanga Princess tayari imeshacheza mechi tatu za Ligi Kuu na kushinda miwili huku ikipoteza mmoja kwa kukubali kichapo cha mabao 3-1dhidi ya Simba Queens, wakati Singida Fountain Gate Princess yenyewe ikishinda mechi mbili na suluhu moja dhidi ya Amani Queens.

Kuelekea mechi ya leo Kocha wa Singida Fountain Gate Princess, Masuod Juma, alisema wachezaji wake wako tayari kwa mchezo wao dhidi ya Yanga Princess kutafuta matokeo chanya katika dimba lao la nyumbani.

Alisema Yanga Princess walikutana nao kwenye Ngao ya Jamii na walipoteza, hivyo hawatakubali kupoteza tena katika mechi hiyo ligi kwa kuwa malengo yao ni kutafuta alama tatu.

"Tumejiandaa vizuri, tunajua ubora wa Yanga Princess, safari hii tutaingia kivingine kusaka alama muhimu za nyumbani, ninaimani na vijana wangu kulingana na maandalizi tuliyofanya kwa ajili ya mchezo wetu wa kesho (leo)," alisema Masoud.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Charles Haalubono, alisema kikosi chake kipo tayari kwa mchezo huo dhidi ya wenyeji wao, Singida Fountain Gate Princess, kutafuta matokeo chanya yenye alama tatu muhimu.

Alisema wamejiandaa kuhakikisha wanarejea na matokeo mazuri ugenini kwa kupata ushindi mkubwa kutoka kwa mpinzani wao huyo.

"Tuko tayari na tunatambua ugumu wa mechi yetu hii, tuna waheshimu Singida Fountain Gate Princess, ninaimani hawatakuja kama walivyocheza mechi zilizopita na watakuja kivingine, tunajua wakiwa nyumbani watahitaji matokeo mazuri kama ilivyo kwetu," alisema Haalubono.

PATASHIKA...



Viungo wa Jamhuri FC, Bulekebe Madeni (kushoto) na Abdul Hafidh Nassor, wakihaha kumdhibiti, winga wa Simba, Luis Miquissone, katika mechi ya robo fainali ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa Uwanja wa New Amaan Sports Complex, visiwani Zanzibar juzi usiku. Simba ilishinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Gamondi apewa panga Yanga SC

INATOKA UK. 24

duzi, wameonyesha thamani ya kuvaa jezi ya Yanga.

„Ila kama kuna mchezaji ambaye hakuonesha kiwango chake katika michuano kama hiyo na kutupa ushindi, sisi Wanayanga tuliomtuma huyo mchezaji kwetu hawezi kuwa na klabu yetu, kocha tumempa mamlaka ya kumwondoa yeyote ambaye anaona hatufai," alisema rais huyo.

Yanga imetolewa kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi hatua ya robo fainali baada ya kuchapwa mabao 3-1 na APR ya Rwanda Jumapili iliyopita.

Baada ya kutolewa, Kocha Mkuu Gambondi alisema mbali na kuwatumia vijana chini ya miaka 20, lakini alitumia baadhi ya wachezaji ambao walikuwa hawapati nafasi katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo kwenye mechi nyingi za Ligi Kuu, achilia mbali Ligi ya Mabingwa Afrika.

Injinia Hersi pia amepinga madai kuwa ana wachezaji wake anaowapenda zaidi kuliko wengine, akisema amehusika na usajili wa wachezaji wote kwenye klabu hiyo.

„Katika wachezaji hawa wa Yanga ninahusika kwa asilimia 99 mpaka 100 kuwasajili, hivyo siwezi kuwabagua wengine na kuwapendelea baadhi.

„Wote nimewasijili mwenyewe, ni mchezaji mmoja tu ambaye sijahusika kwenye usajili wake naye ni Metacha Mnata kwa sababu wakati naingia Yanga nilimkuta, lakini aliondoka na baadaye akarejea tena Yanga na safari hii mimi nikahusika, wote wamepita mezani kwangu, hivyo hakuna mchezaji ambaye kwangu ana thamani kuliko mwingine.

„Mchezaji yeyote anayecheza timu hii ya Yanga ni mchezaji wangu, ninathamini wachezaji wote waliopo hapa bila kujali amesajiliwa na nani," alisema Hersi.

# Bodi yafunguka tarehe ya kurejea tena Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi nchini (TPLB), imesema Ligi Kuu Tanzania Bara inaweza kurejea mapema tofauti na ilivyopangwa awali kama mambo kadhaa yakijitokeza kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zinazotarajiwa kuanza Jumamosi wiki hii nchini Ivory Coast.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, amesema jana kuwa kanuni ndiyo itayoamua kuanza mapema ligi kabla ya AFCON kumalizika na hii itatokana na vitu kadhaa ambavyo vitaangaliwa ikiwamo kama Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kuondoshwa mapema, au kuwapo timu ambazo zina wachezaji pungufu ya watatu kwenye vikosi vyao vya timu ya taifa.

„Kanuni ndiyo itaamua, kwa sasa tunaipisha AFCON, na pia mpaka sasa kuna timu za Ligi Kuu ambazo zina wachezaji zaidi ya watatu kwenye vikosi vya taifa, timu hizi kanuni haziwaruhusu kucheza, ila kama wao watasema wenyewe kuwa wanaweza kuendelea na ligi," alisema Kasongo.

Alisema kama Stars itaendelea kusonga mbele, basi Ligi Kuu Tanzania Bara itasimama mpaka tarehe ambayo imewekwa, lakini vinginevyo basi watafanya utaratibu wa kuirudisha nyuma.

Kama Stars itaendelea kusonga mbele kwa kufanya vema AFCON, Ligi Kuu Tanzani Bara itarejea tena Februari 25 kwa mechi kati ya Ihefu dhidi ya Mashujaa kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya na kuendelea tena Februari 27, mwaka huu kwa michezo mingine mbalimbali.

Kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha AFCON ambapo Timu ya Taifa ya Tanzania inashiriki na Januari 17, saa 2:00 usiku itashuka kwenye Uwanja wa San-Pedro kucheza dhidi ya Timu ya Taifa ya Morocco katika mechi yake ya kwanza ya Kundi F.

Katika hatua nyingine, Kasongo alipongeza Shirikisho la Soka nchini (TFF), wadhamini, wadau wa soka, klabu na waandishi wa habari kwa jinsi walivyoshirikiana na kuifanya Ligi ya Tanzania kuwa kubwa, ikivutia wadau na wachezaji mbalimbali kutoka pande zote za dunia.

Kasongo alisema zamani haikuwa rahisi mchezaji wa kutoka Afrika Kaskazini na Magharibi wenye viwango vya juu kuja kucheza Tanzania, lakini sasa wamekuwa wakimiminika.

„Tuna wachezaji mpaka Wabrazil na Wacolombia, hii ni heshima kubwa kwa taifa letu," alisema Kasongo.

Michezo
Nipashe
Jumatano Januari 10, 2024

Mbappe sasa kuamua mustakabali wake UKURASA 21





# GAMONDI APEWA PANGA YANGA SC

## ●●● Rais amtaka kuanza kufyeka walioboronga Mapinduzi Cup, huku pia akitaka...

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Klabu ya Yanga, Injinia Hersi Said, amesema mchezaji yeyote wa timu hiyo ambaye hakuonesha kiwango katika michuano ya Kombe la Mapinduzi hafai kuichezea timu hiyo.

Rais huyo amempa rungu Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, kuwaacha wachezaji ambao anaona hawawezi kumsaidia katika kutimiza malengo yake na ya klabu katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Hersi amesema Yanga ni klabu kubwa, hivyo haiwezi kukaa na mchezaji ambaye hawezi kuisaidia timu hiyo hata kwenye michuano ya muda mfupi tu kama Kombe la Mapinduzi.

„Nawapongeza waandaaji wa michunao ya Kombe la Mapinduzi, na vijana wetu chini ya miaka 20 ambao wameshiriki Kombe la Mapin-

INAENDELEA UK. 23

# Benchikha sasa amnyima usingizi Chasambi Simba

**Na Saada Akida**

WINGA mpya wa Simba, Ladack Chasambi, amesema anatambua kuwa amejiunga na timu yenye wachezaji wakubwa na anatarajia kupata ushindani mkubwa wa kuwania namba, lakini atahakikisha anajituma mazoezini kwa ajili ya kumshawishi Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, ili awepo kwenye kikosi chake cha kwanza.

Chasambi amesaini mkataba wa miaka mitatu na amejiunga na kikosi cha Simba kilichopo visiwani Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambapo ‚Wekundu wa Msimbazi' hao wametinga hatua ya nusu fainali na leo watashuka dimbani dhidi ya Singida Fountain Gate FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Chasambi alisema amefurahi kujiunga na klabu kubwa ya Simba ambapo mara nyingi kunakuwa na changamoto kwa wachezaji wengi wa kizawa wanapokwenda klabu kubwa, lakini kwake anajiamini na kwamba kitu ambacho kitampa nafasi ni kujituma na bidii ya mazoezi.

Alisema katika nafasi yake kuna wachezaji wengi wenye uwezo ndani ya Simba, lakini anaimani kujiunga ndani ya kikosi hicho ni sahihi kupata vitu vya kujifunza kutoka kwa wakubwa wake ambao wako kwenye kikosi cha Wekundu hao wa Msimbazi.

“Sina hofu juu ya ushindani wa namba uliopo ndani ya Simba, kikubwa natakiwa kujituma kwenye mazoezi na hata mechi nikipewa nafasi ya kucheza ili kuendelea kumshawishi kocha kunipa nafasi ndani ya kikosi chake cha kwanza.

„Ni ngumu kuingia kwenye timu na kupata nafasi moja kwa moja, natakiwa kupambana, kujituma na kushirikiana na wachezaji wenzangu katika mechi na kuhakikisha tunafikia malengo yanayotarajiwa,” alisema Chasambi.

Naye Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema usajili wa winga Chasambi utakuwa na manufaa makubwa kutokana na ubora na umri alionao.

Alisema Chasambi ni mchezaji kijana mwenye kipaji kikubwa kulingana na kile alichokionesha kwenye timu aliyotoka, hivyo baada ya kutua Simba ataingia kwenye kikosi taratibu ili ashinde presha.

“Hatutaki kumpa presha mchezaji wetu kijana, kocha Benchikha ameridhika na usajili wa dogo na tunamuachia afanye kazi yake uwanjani kuonesha kile tunachokitarajia kutoka kwake akishirikiana na wachezaji wenzake,” alisema Ahmed.



Chasambi

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >